TRUTH CENTERED TRANSFORMATION

MODULE



CHUMVI NA NURU

MWONGOZO WA MWALIMU

Truth Centered Transformation is a ministry of Reconciled World. Learn more at tctprogram.org.

Reconciled World

Truth Centered Transformation—Moduli: Chumvi na Nuru v4. Copyright ©2020 Reconciled World, Phoenix, Arizona, United States of America. www.reconciledworld.org

Kazi hii inapatikana kwa kuzingatia masharti ya leseni ya Creative Commons Attribution-ShareAlike 3.0. Unaruhusiwa na kuhimizwa kutumia kazi hii, kunakili, kusambaza, na kuitangaza kwa masharti yafuatayo:

Nukuu - Lazima unukuu kazi hii kwa kusema yafuatayo: Copyright © 2017 Published by Reconciled World (www.reconciledworld.org) under terms of the Creative Commons Attribution–ShareAlike 3.0 license. Kwa taarifa zaidi, angalia www.creativecommons.org.

Kazi hii haiuzwi - Usitumie kazi hii kwa sababu za kibiashara.

Ukiwa na nia ya kutafsiri matirio hii, tafadhali wasiliana na info@tctprogram.org.

Nukuu zote za maandiko matakatifu, zimechukuliwa kwenye Biblia Takatifu, toleo la New International Version®, NIV® Hakimiliki © 1973, 1978, 1984, 2011 by Biblica, Inc.TM. Ikitumika kwa ridhaa ya Zondervan. Haki zote zimehifadhiwa dunia nzima. www.zondervan.com. The "NIV" na "New International Version" ni alama za biashara zilizosajiliwa katika United States Patent and Trademark Office na Biblica, Inc.TM.

Kabla ya kuanza

Maandalizi ya kufundisha somo

1. Usome **Mwongozo wa Mwalimu** kwa uangalifu, mara nyingi iwezekanavyo. Weka alama au andika notsi chini ya mstari kujikumbusha hoja za muhimu.
2. Angalia **malengo makuu** ya kila somo ili ujue mwanafunzi anahitaji kujifunza nini katika somo.
3. Soma aya zote za **maandiko matakatifu** kabla.
4. Angalia uone **matirio** gani inahitajika kwa kila somo na hakikisha unatoa nakala za mwongozo wa mwanafunzi (kopi) na tengeneza picha za vioneshi zinazotumika kwenye somo.
5. Hakikisha unaelewa kila **kitendo/shughuli** katika somo (maigizo, michezo, picha za kujifunzia/vioneshi). Unaweza kufanyia mazoezi na ndugu au marafiki.
6. Tumia muda **kusali/kuomba** ili Mungu awaandae wanafunzi, wasikie kile Mungu anachotaka wasikie, na ili akusaidie kufundisha matirio. Kumbuka kwamba ni kwa njia ya nguvu ya Mungu tu ambayo tutawaona watu wakibadilika

Mwongozo wa Mwalimu

Malengo Makuu na Vifaa: Kila somo linaanza na sehemu hii.

1. **Malengo makuu** –Kuna malengo mazuri mengi katika kila somo, lakini washiriki au wanafunzi wanapaswa kuelewa vizuri malengo haya makuu mwishoni mwa kila somo. Ni vizuri ujiulize ikiwa unafikiria washiriki wanaweza kukumbuka malengo hayo makuu baada ya kufundisha somo. Tumia muda kurudia kuyapitia malengo makuu mara kwa mara ili kuwasaidia kukumbuka.

2. **Vifaa** –Vifaa maalum vinavyohitajika vimeorodheshwa kwa kila somo, pamoja na Vioneshi na Mwongozo wa Mwanafunzi. Mwongozo huu wa Mwalimu utaonesha wakati wa kutumia:
    a. **MWONGOZO WA MWANAFUNZI** – utakuwa umeandikwa hivyo.
    b. **VIONESHI** – vitakuwa vimeandikwa hivyo.

Vioneshi

Vioneshi vya Moduli hii viko katika nyaraka tofauti. Chapisha na utayarishe kama ilivyooneshwa katika ukurasa wa yaliyomo.

Mwongozo wa Mwanafunzi

Ikiwa kikundi chako hakipati kitabu cha Mwongozo wa Mwanafunzi, basi angalau toa kopi/nakala kwa kila mtu za kurasa mbili zilizo mwisho wa Mwongozo wa Mwalimu:

1. Somo la 6: Kushinda Dhambi – Karatasi ya Dhambi za Kawaida
2. Somo la 7: Jedwali la Mpango Wangu wa Kuhudumia

Somo la 1: Chumvi na Nuru

Lengo kuu:

- Kama chumvi, maisha yetu yamekusudiwa kuleta mabadiliko yanayotuzunguka katika jamii zetu.

Vifaa:

- Vioneshi: 'Siwezi kufanya hesabu!' Karatasi ya igizo (zinahitajika nakala 3)
- Chombo chenye chumvi, kijiko
- Mwongozo wa mwanafunzi: Hadithi 3 fupi

Utangulizi: Chumvi

SHUGHULI YA KIKUNDI KIKUBWA
Maelekezo kwa Mwalimu: *shika chombo chenye chumvi au pitisha chumvi darasani watu aione.*

- Hii ni nini?
- Inatumika kufanyia nini? *kutunzia, kuongeza ladha, kutakatishia, kusafishia.*

Chumvi ni ya msingi na njia nzuri ya kuboresha mambo! Kwa kweli, chumvi ni muhimu kwa miili yetu; hatuwezi kuishi bila hiyo.

Yesu aliongea kuhusu chumvi kama ishara jinsi Wakristo walivyo. Leo tunataka kuona jinsi tunavyopaswa kuwa chumvi kwa jamii zetu. Tuanze kwa kuangalia maandiko ili tujue Yesu alivyosema juu ya chumvi.

Wewe ni chumvi

KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO
Soma Mathayo 5:13: 'Ninyi ni chumvi ya dunia. Lakini chumvi ikiwa imeharibika itatiwa nini hata ikolee? Haifai tena kabisa, isipokuwa kutupwa nje na kukanyagwa na watu.

Katika kifungu hiki, Yesu anazungumza na wafuasi wake. Kwa maana sisi ni wafuasi wake, ndiyo maana anatuambia. Wakati wa Yesu, chumvi ilikuwa ya thamani sana. Yesu anawajulisha wafuasi wake kuwa wanathaminiwa sana.

Uwe kama chumvi

Chumvi ilikuwa (na ni) ya thamani kwa sababu ni muhimu sana. Kwa kutulinganisha na chumvi, Yesu anatufundisha kwamba tunaweza kuwa wa muhimu katika jamii zetu. Anaweka wazi kwamba tunaweza na tunapaswa tuwe kama chumvi.

SHUGHULI YA KIKUNDU KIKUBWA *(Tumia **VIONESHI**:* **IGIZO 'Siwezi kufanya hesabu!'**

Wanaohitajika: Muuza duka 1, wanunuaji 2, nafaka ya kuuza.
Tukio: Muuza duka anauza nafaka kwenye duka lake. Mnunuaji anakuja kununua nafaka.

Mnunuaji 1: *(Dukani)* Siku nzuri! Ningependa kununua nafaka. Bei gani?

Muuza duka: Ndiyo, umefika.

(Muuza duka anatoa nafaka, Mnunuaji 1 analipa, muuza duka anampa chenji mnunuaji.)

Mnunuaji 1: *(anaondoka huku anahesabu chenji)* Hii ni siku yangu ya bahati! Muuza duka amenizidishia chenji. Hajaelimika kabisa; hajui hata kujumlisha. HAHA!! **(**Mnunuaji 1 anaondoka).

Mnunuaji 2: (*anafika dukani)* Habari. Nimekuja kununua nafaka.

(Muuza duka anatoa nafaka, Mnunuaji 2 analipa, muuza duka anatoa chenji kwa mnunuaji 2.)

Mnunuaji 2: *(anaondoka huku anahesabu chenji)* Oh hapana! Muuza duka amenizidishia chenji. Amekosea na atapata hasara katika biashara yake kwa njia hii.

Mnunuaji 2: *(anarudi kwa muuza duka)* Samahani. Umenizidishia chenji. (anarudisha pesa iliyozidi).

Muuza duka: Asante sana. Sikumaliza shule na sijui kufanya hesabu vizuri. Jambo hili linaniletea shida kubwa kwenye biashara yangu. Natamani ningeweza kufanya hesabu vizuri.

Mnunuaji 2: Ndiyo, hili ni tatizo. Unajua, ikiwa unapenda kujifunza kweli, ninaweza kukufundisha vizuri ili uweze kuboresha biashara yako.

Muuza duka: Asante sana! Nimefurahi sana kwa kuwa umekuja leo.

- Kati ya hao nani amefanya kama Mkristo anavyopaswa kufanya? *Mnunuaji 2*.
- Mnunuaji 2 alikuwa mwaminifu. Jambo gani lingine mnunuaji 2 alifanya kama Mkristo?
    - *Alijitolea kumfundisha muuza duka hesabu.*
    - *Aliona uhitaji na akafanya mambo yawe bora.*

KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO

Katika moduli zilizopita tulijifunza jinsi maisha yetu yanavyoweza na yanavyopaswa kuboreshwa kwa kufuata njia za Mungu. Sasa tunaona kutokana na shughuli hii na katika maandiko kwamba maisha yetu yamekusudiwa kuleta mabadiliko karibu nasi, katika jamii zetu. Chumvi inapoongezwa, chakula huwa na ladha nzuri. Tunapoenda katika jamii zetu, tunapaswa tuwe tunaboresha mambo kwa wale wanaotuzunguka.

Sisi wote hutumia muda katika jamii yetu kila siku. Hii inamaanisha kwamba mara kwa mara tuna fursa za kuwa kama chumvi kwenye jamii yetu. Vitu tunavyofanya kila siku vinaweza kuonekana si muhimu, lakini kama chumvi-kitu kidogo kinaweza kufanya mabadiliko makubwa.

SHUGHULI YA KIKUNDI KIDOGO

Katika vikundi vya watu 3 au 4 zungumza juu ya njia kadhaa ambazo unashirikiana na watu katika jamii yako. Unawezaje kuwa kama chumvi kwao – kuboresha maisha yao?

KITENDO CHA KUONESHA KATIKA KIKUNDI KIKUBWA

Maelekezo kwa Mwalimu: *Onesha kijiko chenye chumvi.*

Uliza, 'Je, kuna mtu yeyote angependa kula chumvi yote iliyo kwenye kijiko hiki?' *(Hapana!)*

Bila shaka hapana! Chumvi imekusudiwa kuenezwa. *(Onesha kwa kunyunyiza chumvi juu ya sahani, bakuli, au meza.)*

Sisi wote tunahitaji kukumbuka ukweli huu rahisi: Chumvi imekusudiwa kuenezwa. Ikiwa tunajiwekea wenyewe na kuonesha upendo kwa wale walio kanisani tu (kama kuweka chumvi kwenye kijiko), hatutii amri ya Mungu ya kuwapenda wengine (kwa mfano kueneza). Fikiria chumvi inapohitajika. Je, inahitajika zaidi kwenye vitu ambavyo tayari ni vya chumvi? *(Hapana!)* Chumvi ya maisha yetu inakusudiwa kuenezwa kwa wale ambao bado hawajapata chumvi-hasa kwa wale ambao bado hawaamini.

Ikiwa maisha yetu hayaboreshi mambo kwa wale wanaotuzunguka, kwa kweli hatuishi maisha ya Kikristo ambayo Yesu anayakusudia kwetu.

Nuru (au Mwanga)

KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO

Baada ya Mungu kuumba mbingu na dunia, Mungu aliumba kwanza nuru. Kama ambavyo hatuwezi kuishi bila chumvi, pia hatuwezi kuishi bila nuru. Ni muhimu kwa maisha yetu.

- Nuru hufanya nini?

    - *Inaleta uhai, huonesha rangi na uzuri, huonesha hatari zinazowezekana.*
- Fikiria kusingekuwa na mwanga wa jua, hakuna umeme, hakuna mwanga wa mwezi. Maisha yangekuwaje?
    - *Hakuna kitu ambacho kingekua.*
    - *Tusingeweza kuona kabisa, tusingeona hata mita 1 mbele yetu.*

Soma Yohana 8:12

- Nani ni nuru ya ulimwengu?
    - *Yesu*
- Tunapomfuata Yesu kinatokea nini?
    - *Hatutembei gizani, hatuwi vipofu, tunaweza kuona tunakoenda.*
    - *Tuna nuru/mwanga wa maisha, tuko hai kiroho na tunakua.*

Yesu anasema yeye ni nuru ya ulimwengu na kwamba tunaweza kuwa na nuru hiyo kwa kumfuata.

Soma Mathayo 5:14–16.

- Nani ni nuru ya ulimwengu katika mistari hiyo?
    - *Wafuasi wake—ambao ni sisi!*
- Yesu anasema tunahitaji kufanya nini ili 'kuiangaza nuru'?
    - *Matendo mema*
- Nuru ni kwa ajili ya nani?
    - *Kila mtu ndani ya nyumba, watu wote*
- Kulingana na maneno ya Yesu, kitatokea nini tutakapoiangaza nuru ya ukweli?
    - *Watu wengine wataona matendo yetu mema na kumsifu Baba yetu wa mbinguni, kuleta utukufu kwa Mungu.*

Mungu amelipa kanisa (yaani, Wakristo) jukumu maalum ulimwenguni: kuwa nuru! Yesu aliwapitishia wafuasi wake nuru ya upendo wake. Bila kanisa hakuna nuru nyingine; kuna giza tu. Popote watu wa Mungu wanapochagua kutoiangaza nuru yao, jamii zao zinaachwa gizani. Bila nuru ya maisha, hakuna tumaini kwa jamii zetu.

Hadithi za makanisa ya Chumvi na Nuru

SHUGHULI KATIKA KIKUNDI KIDOGO

Maelekezo kwa Mwalimu: *Gawanya vikundi 3. Awepo msomaji 1 katika kila kikundi. Kila kikundi kisome hadithi MOJAWAPO katika* ***MWONGOZO WA MWANAFUNZI*** *na jibu maswali. Waeleze kwamba hadithi hizi ni za ukweli kabisa kuhusu kijiji halisi. Halafu na vikundi viwasilishe hadithi na majibu kwa kikundi chote.*

Jamii ya 1 Katika kijiji kimoja, mtu alipougua, mganga alikuja na kuwataka watoe kafara ya mnyama ili apate ushauri na dawa. Wakristo walipojifunza kanisani juu ya afya kupitia programu ya TCT, walianza kutumia masomo hayo kujitibu magonjwa ya kawaida na majirani zao. Watu wote kijijini waliweza kuona kwamba watu waliokuwa wakifuata ushauri wao wangepona bila hata kutoa kafara ya wanyama. Sasa kijiji kizima kinajaribu kuzuia na kutibu magonjwa badala ya kutoa kafara. Hii huokoa pesa zao na kuwafanya wawe na afya! Inaonekana kwamba kumtumikia Mungu kunaboresha zaidi maisha ya Wakristo. Kunaboresha maisha ya wengine, pia!

Jamii ya 2 Katika kijiji kimoja, watu walipokuja kuvuna shambani, mmiliki wa shamba angelazimika kuandaa chakula kingi na soda au pombe kwa watu waliosaidia. Pengine gharama ya hii ilikuwa kubwa zaidi ya faida kutoka kwenye mavuno! Baada ya kusoma juu ya kufanya Matendo ya Upendo, Wakristo katika jamii hii waliamua kwamba watasaidia katika mashamba ya maskini bila malipo yoyote. Watu walishangaa kwamba Wakristo hawakusaidiana wenyewe tu bali walisaidia watu nje ya kanisa pia. Mara, watu wengine kijijini waliona kile walichokuwa wakifanya na wakaacha kuhitaji chakula na vinywaji, pia. Sasa kila mtu kijijini yuko

tayari kufanya kazi kwenye mashamba ya wengine bure. Wote huleta vyakula vyao, na hufanya kazi kwa pamoja. Matokeo yake, kila familia ina uwezo wa kupata faida. Sasa msimu wa kuvuna ni wakati ambao kijiji kinatarajia badala ya kuuhofia, na wanaweza kuhudumia familia zao kwa faida zao wanazopata.

Jamii ya 3 Kijiji kimefanya Matendo ya Upendo kuwa sehemu ya maisha yao ya kila siku. Wanafanya Matendo ya Upendo kila wiki. Kwa kweli, huu umekuwa utaratibu wa kawaida katika maisha hivi sasa, mtu anapoona uhitaji, wataacha kile wanachofanya na kujaribu kutatua shida. Kukiwa na mawe au takataka barabarani, huziondoa. Kijiji chao kilikuwa ni moja ya vijiji vichafu zaidi, na maendeleo duni katika eneo hilo. Lakini sasa ni kisafi na kinatunzwa vizuri. Hivi karibuni wameweza kujenga kanisa zuri kwa mapato yanayotokana na kufanya kazi kwa bidii na kusaidiana! Mabadiliko hayo yanaonekana kwa wote wanaopita kijijini. Lakini yanaweza pia kuonekana kwa jinsi ambavyo wanakijiji hutendeana. Kila mtu kijijini anafurahi zaidi na anashukuru kwamba watu wa kanisa waliwapenda vya kutosha kuwaonesha njia bora ya kuishi.

- Katika hadithi hii kanisa lilifanya nini?
- Mabadiliko gani yalitokea kwenye jamii?
- Watu katika kijiji walichukuliaje?
- Mtazamo wao kwa kanisa ni upi?
- Tunawezaje kuwa kama kanisa hili?

TOA RIPOTI

Mungu anataka kuona jamii zetu zikiponywa. Kutoka kwenye maandiko na hadithi zetu za leo, tunaweza kuona kwamba matumaini ya uponyaji wa jamii zetu yamo kanisani — ulimwengu hauwezi kuleta uponyaji. Sisi ni nuru inayoweza kufukuza giza katika jamii yetu!

- Je, unaweza kushirikisha hadithi kutoka katika jamii yako zinazoonesha jinsi kuangaza nuru ya maisha kulivyoleta mabadiliko kwa majirani zako?
- Je, kuna Matendo ya Upendo yoyote yaliyoleta mabadiliko katika jamii yako?
- Je, Matendo yako ya Upendo yamewafikia wale walio nje ya kanisa?
- Ni jambo gani lingine unaweza kulifanya kama kanisa kuleta nuru kwa jamii yako?

Hitimisho

Tumia muda kidogo ujiulize: Je, kweli ninaamini kwamba Mungu amekusudia wafuasi wake - pamoja nami na kanisa langu - kuleta mabadiliko katika jamii yetu?

Uombe kwamba Mungu atusaidie kuamini kwamba anataka kuwa mwenye nguvu kazini kupitia sisi kuleta nuru gizani katika jamii zetu. Mwombe Mungu akuoneshe njia ambayo angekutumia kama chumvi na nuru, kisha umsubiri kwa utulivu ajibu.

Somo la 2: Kumtukuza Mungu

Malengo makuu:

1. Kusudi la kuwa chumvi na nuru kwa wengine ni kumtukuza Mungu.
2. Tunapaswa kumtukuza Mungu katika yote tunayofanya.

Vifaa:

- Hakuna

Utangulizi: Wa thamani kwa Mungu

Kabla ya kuendelea, tujikumbushe tuliyojifunza katika Somo la 1
Soma Mathayo 5:16: 'Vivyo hivyo nuru yenu iangaze mbele ya wengine, ili wapate kuona matendo yenu mema na kumtukuza Baba yenu aliye mbinguni.'

- **Kwa nini tuiangaze nuru yetu kwa kuwafanyia watu wengine matendo mema?**

Lengo la kufanya matendo mema- ya kuwa chumvi na nuru na kufanya Matendo ya Upendo-ni ili wengine wamsifu Mungu! Tunafanya Matendo ya Upendo ili Mungu atukuzwe. Katika somo hili, tutaona ni kwa nini utukufu wake ni lengo letu la muhimu zaidi.

Maisha yetu yanabidi yamtukuze Mungu

KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADIIANO
Leo tutasoma kifungu kutoka Agano la Kale. Katika kifungu hiki, Waisraeli — watu waliochaguliwa na Mungu — walikuwa wametoroka kutoka utumwani na walisafiri kwenda nchi ambayo Mungu aliwaahidi. Ilikuwa safari ndefu jangwani. Walipofika ukingoni mwa nchi ambayo Mungu alikuwa amewaahidi, walituma wapelelezi katika nchi hiyo ambao waliona kwamba ilijazwa na vitu vingi vizuri-kama mafungu ya zabibu ambayo yalikuwa makubwa sana watu wawili waliweza kubeba. Lakini pia waligundua shida — kulikuwa na majeshi mengi yenye nguvu katika nchi hiyo. Wapelelezi wawili walitoa ripoti nzuri juu ya mambo mazuri lakini wengine walisema kuhusu matatizo tu. Hebu tusome katika Hesabu kile kilichotokea.

Soma Hesabu 14:1–20.

Katika kifungu hiki, watu wa Israeli walitenda dhambi. Badala ya kuamini ahadi za Mungu alizowaahidia, walilalamika dhidi ya Musa na dhidi ya Mungu, wakisema wangekuwa heri ikiwa wangekaa watumwa Misri au wangekufa jangwani (mstari 1-4). Kwa kujibu, Mungu anasema kwamba atawaangamiza Waisraeli na badala yake atatengeneza kabila kutoka kwa Musa. Musa anaenda kwa Mungu na kumsihi asifanye hivyo.

- Katika aya ya 13-16, Musa anatoa sababu gani ya kumwomba Mungu asifanye hivyo?
    - *Mataifa mengine yatasikia habari hiyo na kusema Mungu hakuweza kutimiza ahadi zake.*
- Musa anajali nini?
    - *Sifa ya Mungu, watu wengine wataamini nini juu ya Mungu.*

Musa ana wasiwasi kwamba Mungu akiwaangamiza Waisraeli, basi Wamisri watafikiria kwamba Mungu hakuweza kutimiza ahadi yake ya kuwaleta katika nchi ya ahadi. Musa anajali sifa ya Mungu-utukufu wake! Anajiuliza, 'Je, wale wasio Wakristo watafikiria nini juu ya Mungu likitokea hili?' Musa hasemi, 'Usiwaangamize Waisraeli kwa sababu sisi ni watu wazuri,' au 'kwa sababu hiyo nitaonekane kama kiongozi mbaya.' Hangaiko kuu la Musa ni sifa ya Mungu.

- Je, umewahi kufikiria sifa ya Mungu?
- Je, sisi kama Wakristo tunapaswa kukumbuka sifa ya Mungu (yaani, utukufu wake?)? Kwa nini au kwa nini hapana?

Soma 1 Wakorintho 10:31.

- Kulingana na Paulo, ni wakati gani tunapaswa kujali utukufu wa Mungu?
    - *Tunapofanya kitu chochote - hata kazi rahisi, kazi za kila siku za kula na kunywa.*
- Ikiwa nyumba za Wakristo ndizo zinatunzwa vibaya katika jamii, mali zao hazitunzwi, na watoto wao wamevaa nguo chafu, unafikiri watu wa jamii hufikiriaje kuhusu Mungu?
    - *Wanaweza kujiuliza ikiwa Mungu anaweza kuwajali watu wake, wanaweza kuamini kwamba Mungu anajali tu mambo ya kiroho lakini hajali familia.*
- Je, hii inamaanisha kwamba tunahitaji kuwa matajiri au wakamilifu kumtukuza Mungu ili watu watupende?
    - *HAPANA! Kwa hakika, Yesu mwenyewe alizaliwa katika familia iliyokuwa maskini. Walakini, tunahitaji kutumia vyema kile Mungu alichotupatia. Tunahitaji kutumia rasilimali na ujuzi tulio nao kumletea Mungu heshima.*

Tumeitwa kumletea Mungu utukufu katika yote tunayofanya. Hapa kuna hadithi ya kuelezea jinsi inavyoweza kuonekana.

> Kulikuwa na familia iliyohamishiwa kwenye kambi ya wakimbizi kwa sababu ya vita nchini mwao. Kabla ya vita, familia hiyo ilikuwa tajiri sana. Sasa wametoka kuishi katika nyumba ya kifahari na kuishi kwenye kibanda cha matope. Mke hakujali nyumba duni na haraka ilianguka. Aliikumbuka nyumba nzuri aliyokuwa nayo na aliweza kufikiria tu yale ambayo hakuwa nayo. Baada ya muda, Shemeji yake mkubwa alikuja kukaa. Alifagia na kusafisha eneo hilo, alikarabati nyumba, na akachukua maua ili kuleta uzuri wa Mungu kidogo ndani. Alikaa kwa wiki chache akifanya aina hizi za kazi rahisi bila kutumia pesa yoyote. Kwa kuongeza mimea na maua na kuifanya nyumba iwe nadhifu, safi na isiyo na msongamano, hisia ndani ya nyumba ilibadilika. Hii ilitoa tumaini sio tu kwa mke wa kaka yake, bali kwa familia nzima na majirani zao pia. Ingawa familia ilikuwa bado maskini na nyumba ilikuwa bado ndogo na ya hali ya chini, ndugu huyo alitumia kile ambacho familia ilikuwa nacho kumtukuza Mungu katikati ya hali ngumu.

SHUGHULI YA KIKUNDI KIDOGO

Katika vikundi vidogo, toa mawazo mengi iwezekanavyo kwa maswali haya 2.

Maelekezo kwa Mwalimu: *Ikilazimika, anza kwa kutoa mawazo machache pamoja ili waelewe majibu gani yanawezekana. Vikundi vikimalizika, vitoe ripoti kwenye darasa.*

Ni njia gani tunazoweza kujenga sifa ya Mungu kati ya wasio Wakristo?	Ni njia gani ambazo tunaweza kuharibu sifa ya Mungu miongoni mwa wasio Wakristo?
• *Kuwatunza watoto wetu* • *Kuwapenda wake zetu* • *Fanya kazi kwa bidii* • *Watumikie wengine* • *Fuata maagizo ya kiafya* • *Tunza mazingira, wanyama, mifugo* • *Kuweka vitu vyetu vizuri*	• *Kutotunza familia zetu* • *Kuharibu mazingira* • *Kutojali miili yetu(kunywa pombe&Kuvuta sigara)* • *Kukasirika kwa haraka* • *Kutokuwa waamini (katika mambo ya kila siku/ biashara)* • *Kutokuwa mwaminifu kwa mke/mume wako* • *Kupiga watoto, mke, wanyama*

TOA RIPOTI

KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO

- Watu wanapoangalia maisha yako, je, wanafikiria, ‘Mungu ni wa kustaajabisha sana. Sheria zake ni kwa faida yetu. Njia zake ni bora! ’Au wanafikiri kwamba Mungu wetu hana nguvu sana au si wa muhimu sana?
- Je, tunamtii Mungu katika kila eneo la maisha yetu? Je, tunafanya kazi kwa bidii? Je, tunawatendea wengine kwa upendo? Je, tunatumia pesa zetu vizuri? Je, sisi ni waaminifu? Tunatoa kwa ukarimu? Tunaweza kufanya nini tofauti?

Mabalozi wa Mungu

KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO
Sifa ya Mungu ni muhimu sana. Ametuita mabalozi wake.

Soma 2 Wakorintho 5:20.

- Mjumbe au Balozi ni nani?

Maelekezo kwa Mwalimu: *Badilisha nchi kwa kuweka nchi zinazojulikana kulingana na hadhira.*

Balozi ni mtu ambaye huenda kutoka nchi moja kwenda nyingine kuwakilisha nchi yao. Kwa mfano, huko Marekani kuna balozi wa Kenya. Anawajibika kuiwakilisha Kenya nchini Marekani. Serikali ya Kenya ikifanya maamuzi yoyote, basi balozi huzungumza kwa niaba yao huko USA. Anawaambia watu kuhusu utamaduni na watu wa Kenya. Anawahimiza kutembelea Kenya, kuanzisha biashara nchini Kenya, na kununua bidhaa za Kenya. Anawakilisha pia Kenya kwa kuhudhuria hafla na kuonekana hadharani — kila kitu anachosema na kufanya, hata jinsi anavyovaa, inakusudiwa kuleta heshima na faida kwa nchi yake.

Sisi pia ni mabalozi, lakini kwa ufalme wa Mungu. Watu wanapotuangalia sisi na maisha yetu, wanapaswa kuona jinsi ufalme wa Mungu ulivyo.

- Je, maisha yetu huwaambia nini watu kuhusu ufalme wa Mungu ulivyo?

Fikiria jinsi ulivyomwakilisha Mungu wiki iliyopita. Watu wanapotazama maisha yako, wanaweza kuelewa nini kuhusu Mungu ni nani?

SHUGHULI NA MWENZAKO
Katika jozi ya watu wawili fikiria juu ya mambo mtakayojaribu kufanya wiki hii. Ombeni pamoja ili Mungu awasaidie kufanya mabadiliko mnayotaka kufanya.

Hitimisho

Kuishi kwa utukufu wa Mungu kunaweza kutujaza furaha katika hali zote.

Katika Yohana 15: 10-11, Yesu anasema, "Mkizishika amri zangu, mtakaa katika pendo langu… nimewaambia haya yote ili furaha yangu iwe ndani yenu na furaha yenu iwe kamili." Kuzishika amri za Yesu sio mzigo mzito, lakini ni furaha!

1 Petro 2:12, inasema, 'Ishi maisha mazuri kati ya [wale ambao hawaamini] ili, ingawa wanakushutumu kwa kufanya vibaya, waone matendo yako mema na wamtukuze Mungu siku atakayotutembelea.'

Lengo letu la kuishi katika utukufu wa Mungu ni kwamba wengine wamtukuze, pia. Je, sio jambo jema kwamba kwa kuishi kwa njia hii, Mungu hutubariki na zaidi kwa kutupa furaha?

Somo la 3: Ukristo wa kweli

Lengo makuu:

1. Ukristo wa kweli unatokana na vile tulivyo kwa ndani, sio shughuli zetu za nje. Shughuli hizi zinapaswa kuwa matokeo ya upendo wetu kwa Mungu.

Vifaa:

- Vioneshi: Wahusika 3 kadi za maelekezo ya igizo
- Mishumaa 3 na viberiti (shughuli ya hiari)

Utangulizi

KIKUNDI KIDOGO CHA MAJADILIANO

- Unawezaje kumwelezea Mkristo wa kweli? Unawezaje kumtambua mtu aliye Mkristo wa kweli? Orodhesha vitu wanavyofanya au sifa wanazoweza kuwa nazo.

TOA RIPOTI

Maelekezo kwa Mwalimu: *Waambie watu washirikishe baadhi ya sifa walizoziandika. Kisha waambie waangalie orodha zao. Ni mambo mangapi kwenye orodha ni shughuli kama kuhudhuria kanisani? Kuna mambo mangapi ya tabia kama kuwa mwaminifu? Orodha ipi ni kubwa?*

Leo tutaangalia mifano 3 ya kawaida ya tabia ya Mkristo.

Mhusika wa 1: Kwa nje tu

SHUGHULI YA KIKUNDI KIKUBWA: IGIZO

Maelekezo kwa Mwalimu: *Utahitaji watu 3. Unapotoa karatasi za* ***VIONESHI*** *za igizo hakikisha watu waliojitolea wako tayari kuigiza kwa namna zifuatayo:*

– Mhusika wa 1: Igiza wa kujivunia sana
– Mhusika wa 2: Igiza kwa kuhukumu na kukasirika
– Mhusika wa 3: Igiza kwa kujali, unyenyekevu, na kutubu.

Mhusika wa 1: (Igiza kwa KUJIVUNIA)

Ni furaha ilioje! Leo nilihubiria mjini katika umati wa watu. Spika zangu zilikuwa muhimu sana kwa kila mtu kusikia maombi yangu muhimu na sheria za kiroho. Niliwaambia njia zote wanazopaswa kuziishi. Najua niliwatumainisha, kwa sababu wote waliinua mikono yao kuwa Wakristo nilipomaliza kuhubiri. Kwa kweli mimi ndiye mwinjilisti bora katika eneo hili — hakuna mtu mwingine aliye na mafanikio kama mimi! Haishangazi: Mimi hutumia masaa 2 kuomba na saa 1 kusoma Biblia kila siku. Wiki iliyopita nilifunga kwa siku 3 na nikamwomba Mungu anipe watu 150 watakaookoka mwezi huu. Nina hakika anapoona ni kiasi gani ninaomba na kufunga hivyo, atajibu maombi yangu. Ni vibaya sana kwamba wengine sio wa kiroho kama mimi. Hawajui jinsi ya kujitolea kwa dhati kwenye kazi ya Mungu… Oh! yule mlevi wa kitongoji jirani tena. Inaonekana hata hataweza kuijua njia ya kurudi nyumbani na sasa ni saa 11:00 tu! Anahitaji kusikia moja ya mahubiri yangu! Kweli, sina muda kwa ajili yake sasa hivi - ni muda wa kuomba! (Anaharakisha.).

- Unawezaje kumwelezea Mhusika wa 1?
    - *Anajali utukufu wake tu; anavutiwa na mambo ya kiroho, sio Matendo ya Upendo.*
- Je, umewahi kukutana na mtu kama huyo?

Mhusika wetu wa kwanza ni kama Mfarisayo. Mafarisayo walikuwa viongozi wa kanisa wakati wa Yesu. Walijitolea maisha yao yote kusoma na kufundisha Sheria ya Musa. Walijali sana kufuata sheria za Mungu na kuishi kikamilifu 'maisha matakatifu' hivyo waliongeza marufuku zaidi 365 na amri 250 kwenye Amri 10 na walitarajia kila mtu kuzifuata. Mafarisayo walidhaniwa kuwa watu watakatifu zaidi. Mtu wa kawaida asingeweza kamwe kuwa 'mtakatifu' kama wao.

Hata hivyo, tena na tena katika Biblia tunaona Yesu akiwakosoa Mafarisayo walionokana kuwa 'watakatifu zaidi.' Kwa kweli, maneno makali ya Yesu hayakuwa kwa watu kama makahaba au walevi bali kwa Mafarisayo. Hebu tusome yale aliyowaambia:

Soma Mathayo 23:1–7, 23–28.

- Kutoka kwenye mistari hiyo, unafikiri dhambi ya Mafarisayo ilikuwa ipi?
    - *Mafarisayo walikuwa na matendo yote sahihi, lakini kwa ndani walikuwa wenye tamaa, wenye kiburi, walijipenda wao tu, na kujitangaza.* ***Hawakujali watu*** *lakini waliweka viwango vikali, sio viwango vya Mungu. Watu hawakuweza kufikia viwango walivyoweka. Ingawa hawakuwa wakamilifu,* ***walitenda kana kwamba walikuwa wakamilifu na walihukumu vikali kila mtu ambaye hakuwa mkamilifu. Mafarisayo hawakuwa na wasiwasi juu ya kuishi maisha matakatifu kama walivyokuwa wakionekana kuwa Watakatifu.***

Wakati Mafarisayo na mhusika katika igizo letu ni mifano mikubwa, sisi sote tunaweza kujaribiwa kujifanya kuwa sisi ni wa kiroho zaidi kuliko vile tulivyo, au tu kutenda kama Mkristo wakati tuko mbali sana na Mungu. Mungu havutiwi na kile tunachofanya nje kwa kuwa yeye yuko katika uhusiano wetu na yeye. Matendo yetu ya nje yanapaswa kutoka kwenye uhusiano wa karibu naye.

Sasa tumwangalie mhusika wetu wa pili.

Mhusika wa 2: Kuhudumia Bila Upendo

SHUGHULI YA KIKUNDI KIKUBWA: IGIZO
Maelekezo kwa Mwalimu: *Tumia kadi za* ***VIONESHI***

Mhusika wa 2: (Igiza umefadhaika, mtazamo mbaya, na ukasirike unapoongea) :
Huh! Siku ilioje. Nimechoka! Kuwa sehemu ya kanisa kunatumia muda wangu mwingi! Kila wiki natumia muda wangu kusaidia wengine. Haishangazi mchungaji aliniambia kwamba nilikuwa baraka kubwa kwa kanisa! Leo nilitembelea watu 3 waliokuwa wagonjwa na kuwaletea chakula. Wiki iliyopita tu, nilipangilia nyumba ya mjane… (Anaanza kukasirika) Sio kwamba namfahamu mwanamke huyo. Namaanisha kwamba hakushukuru sana. Alisema Asante, lakini ilionekana kana kwamba anastahili. Hakika sipendi watu kama hao. Hawaelewi kile ninachotoa sadaka kuwasaidia. Ninamaanisha nina familia yangu ya kutunza. Lakini kwa kweli hakuwa na shukrani. Watu wanapaswa kuheshimu juhudi zangu zaidi. Mjane mjinga, natamani nisingemsaidia.

- Unaweza kumwelezeaje Mhusika wa 2?
    - *Anafanya kazi kwa bidii kwenye shughuli za kanisa lakini kwa mtazamo na nia mbaya.*

Mhusika wa pili alijali kuhusu sifa yake. Alikuwa akifanya Matendo ya Upendo kwa mtazamo mbaya na kwa sababu mbaya-ili wengine *wamsifu*. Ngoja tuangalie kifungu kingine kinachozungumzia shida hii.

Soma 1 Wakorintho 13:1–3.

- Kutoka kwenye maandiko, jambo gani lilikosekana kutoka kwa mhusika wa pili? (*upendo)*

Biblia inatufundisha wazi kuwa kuwatumikia wengine bila upendo ndani ya mioyo yetu haitoshi! Tunaelewa kutoka katika kifungu hiki kwamba lazima tuwe na upendo ili Matendo yetu ya Upendo yafae.

KIKUNDI KIDOGO CHA MAJADILIANO
Fikiria mtu wa 2 amekuja kwako kuomba ushauri. Alikuwa amesikia mahubiri juu ya 1 Wakorintho 13 lakini hakuhisi upendo. Alitaka kupenda lakini alitakiwa awapendaje watu wengine? Hasa wale waliokuwa wanasumbua au kumwudhi. Ushauri gani ungempa Mtu wa 2 kuhusu namna ya kukua katika kuwapenda wengine?

TOA RIPOTI

Chanzo cha Upendo

Tukitaka kukua katika upendo, daima lazima tuende kwenye chanzo cha upendo.

Soma 1 Yohana 4: 7–9.

- Upendo unatoka wapi? *Upendo hutoka kwa Mungu. Mungu ni upendo*

Kwa kuwa upendo unatoka kwa Mungu tunahitaji kumtazama Mungu ili atupatie upendo zaidi tunapokuwa hatuhisi upendo.

ONESHO KATIKA KIKUNDI KIKUBWA (HIARI)
Maelekezo kwa Mwalimu: *Chagua mtu aliyejitolea aje mbele. Mpe mshumaa usiowashwa. Mwelekeze mtu huyo kuwasha mshumaa. (Haitawezekana kuuwasha bila chanzo cha moto au kiberiti.)*

Uliza:

- Kwa nini huwezi kuuwasha mshumaa wako?
    - *Kwa sababu sina kiberiti cha kuwashia.*
- Unahitaji nini?
    - *Kiberiti / chanzo cha moto.*

Maelekezo kwa Mwalimu: *Mwambie aliyejitolea abaki mbele. Mpe mtu mwingine mshumaa mwingine usiowashwa humo darasani. (Haitawezekana pia kwa sababu bado hakuna chanzo cha moto/kiberiti).*
Uliza:

- Kwa nini huwezi kuwasha mshumaa wa jirani yako*? Kwa sababu mshumaa wangu haujawashwa.*
- Je, inaleta maana kujaribu kuwasha mshumaa wa mtu mwingine bila ya mshumaa wako kuwaka? *Bila shaka hapana!*

Kama vile tusivyoweza kuwasha mshumaa bila chanzo cha moto au taa, sisi pia hatuwezi kujazwa kweli na upendo bila chanzo cha upendo.

Maelekezo kwa Mwalimu: *Juu ya meza mbele ya darasa, washa mshumaa mkubwa.*

- *Sema*, 'Yesu ndiye Nuru / mwanga wa ulimwengu. Chanzo cha mwanga au nuru yetu kinatoka kwa Mungu kupitia Yesu Kristo. '
- *Mwulize mtu wa pili aliyejitolea, 'Ukija kwenye chanzo hiki cha mwanga, unaweza kuwasha mshumaa wako?' (Ndiyo.)*
- *Mwelekeze mtu huyo awashe mshumaa.*
- Sema, 'Sasa umejazwa na nuru kwa sababu ulikuwa unatafuta chanzo cha nuru. Je, sasa unaweza wa kuwasha mshumaa wa jirani yako? '(*Ndiyo.)*

- *Mwambie mtu aliyejitolea awashe mshumaa mwingine.*
- Tunajifunza nini kutoka kwenye onesho hilo?
    - *Yesu ndiye mwanga na chanzo cha upendo wetu. Hatuwezi kupenda vizuri bila kupokea upendo wake.*

Ni wazi kwamba lazima tuende kwenye chanzo cha upendo ili tukue katika upendo ili tuweze kuwaonesha wengine upendo wa Kristo.

Kukua katika Upendo

Kama tulivyosema tunaweza kukua katika upendo kwa kuomba na kumwomba Mungu aongeze upendo wetu. Hapa kuna mawazo mengine.

1. WAOMBEE WENGINE
    - Upendo unakua tunapowaombea watu — hata wale tusiowapenda. Mwombe Mungu akupe upendo kwao. Unapotumia muda kuwaombea kila siku utashangaa jinsi Mungu anavyobadilisha mtazamo wako kwao. Hii huchukua muda!
2. FANYA / TII
    - Upendo hukua tunapotenda; upendo sio hisia nzuri tu. Wakati mwingine ni kitendo. Kwa hivyo, hata ikiwa sio lazima tujisikie upendo, bado tunaweza kujaribu kuonesha upendo kwa mtu na kuomba kwamba hisia ya upendo ikue.
3. TUMIA MUDA KUJIFUNZA KUHUSU WENGINE
    - Mara nyingi tunapojifunza zaidi juu ya wengine ndipo upendo wetu kwao huongezeka.

Kumbuka: kumpenda mtu haimaanishi kwamba unakubaliana na matendo yao yote. Ikiwa mtu anatenda dhambi, basi hatukubaliani na dhambi hiyo, lakini tunampenda mwenye dhambi. Yesu alitumia wakati wake na makahaba na watoza ushuru na wengine waliofanya maovu ya kijamii. Hakukubali dhambi yao, lakini aliwapenda. Alikula nao, akashirikisha maisha yake pamoja nao na aliwahudumia kwa upendo wake mkubwa.

Mhusika wa 3: Kuhudumia kwa Moyo uliojaa Upendo

SHUGHULI YA KIKUNDI KIKUBWA: IGIZO
Maelekezo kwa Mwalimu: *Tumia kadi za* ***VIONESHI***

Mhusika wa 3: (Igiza kwa unyenyekevu na Toba/kutubu)
Mimi nimevutiwa sana na (mtu wa 1) na (mtu wa 2). Wao ni wa kiroho sana na hufanya mambo mengi mazuri kwa kanisa. Lakini inaonesha kama siwezi kamwe kuwa vizuri kama wao. Leo nilijaribu kutumia muda kuomba, lakini baada ya dakika chache tu, binti yangu alianguka na kuumia gotini, hivyo niliacha kuomba na kwenda kumsafisha na kuweka bandeji kwenye kidonda. Mara ukafika muda wa kuwapeleka watoto shuleni. Baada ya hapo, nilienda kufanya kazi shambani. Nilipokuwa nikirudi nyumbani, nilimtembelea mjane aliye karibu. Mwanamke huyo-amefiwa mumewe hivi karibuni, na ana uchungu sana. Ninamwonea huruma sana. Tulitumia masaa machache kuzungumza huku nikimsaidia kufua nguo, na nilisali naye. Alionekana kuwa na furaha zaidi, lakini ningetamani kwamba kungekuwa na mambo zaidi ambayo ningeweza kufanya kumsaidia. Moyo wangu unamsikitikia sana. Ningekuwa wa kiroho zaidi kama wale wengine, basi ningeweza kufanya zaidi.
(Anainamisha kichwa) Baba, naomba unisamehe kwa njia ambazo si mkamilifu. Nataka kuishi maisha ambayo yanakupendeza. Nioneshe namna ya kutumia muda wangu na jinsi ya kuwapenda wengine vile unavyotaka. Ninahitaji msaada wako; Najua siwezi kufanya peke yangu.

- Unawezaje kumwelezea mhusika wa 3?

    - *Mnyenyekevu, anajali, kuonesha upendo ni sehemu ya maisha ya kila siku. Yeye ni chumvi na nuru/mwanga wa kweli.*
- Alitumiaje muda wake? *Kufanya Matendo ya Upendo, kutamani kutumia muda katika maombi.*
- Unajuaje alikuwa na moyo uliojaa upendo*? Alimhurumia jirani, akatafuta utukufu wa Mungu.*

KIKUNDI KIDOGO CHA MAJADILIANO
Soma Luka 18:9-14
- Nani alimsifu Mungu katika kifungu hiki?
- Jambo gani lilikuwa linashangaza kuhusu hili? (Kumbuka kile tulichojifunza kuhusu Mafarisayo.)
- Ni igizo lipi kati ya maigizo hayo matatu unafikiria linafafanua zaidi aina ya Mkristo ambaye Mungu anamtafuta? Kwa nini?
- Angalia tena maelezo yako ya asili ya Mkristo wa kweli. Je, unaweza kurekebisha vipi kutokana na yale ambayo tumeona hadi sasa katika somo hili?

Mhusika wa tatu alifanya kazi zake za kawaida, za kila siku waa moyo uliotaka utukufu wa Mungu. Hakuwa na sifa maalum na hakuwa maarufu kama mtu wa kipekee, lakini alikuwa na moyo uliojaa upendo na roho ambapo alikuwa tayari kutenda kwa upendo. Alifanya kwa ukarimu na akamtafuta Mungu kwa maombi. Alikuwa mwaminifu kwa kazi yake ya kila siku na bado alijibu mahitaji yaliyomzunguka. Mhusika wa tatu anaonesha kwamba hatupaswi kuwa wakamilifu ili tutumikie! Mungu anatamani tumpe kile tulicho nacho (maisha yetu ya kila siku) kwa utukufu wake.

Kuwahudumia wengine kwa mioyo iliyojaa upendo ndivyo humletea Mungu utukufu na kusababisha wengine kumsifu! Hatuwezi kuwa nuru ya ulimwengu bila moyo uliojaa upendo. Njia pekee ya kuwa na moyo uliojaa upendo ni kutafuta utukufu wa Mungu badala ya sisi wenyewe.

Hitimisho

Katika masomo machache yaliyopita tumekumbuka tena mengi ya matendo ya Mkristo-tunapaswa kuwa chumvi na mwanga, na kumletea Mungu utukufu. Lakini kamwe hatupaswi kusahau kwamba uwezo wa kufanya mambo haya unatoka kwa Mungu. unaanza na uhusiano mzuri na Mungu. Bila hivyo tutakuwa kama wahusika wawili wa kwanza - ama kufanya tu mambo ya sahihi ya nje huku uko mbali na Mungu au kumtumikia lakini hukosa upendo na kuwa na kinyongo.

TAFAKARI BINAFSI
Wafikirie tena wahusika katika maigizo yetu-wewe ni kama nani? Mwombe Mungu achunguze moyo wako na akuoneshe majibu ya maswali yafuatayo:
- Je, ninataka Mungu apokee utukufu na sifa kwa sababu ya kile ninachofanya? Au ninajali zaidi juu ya wengine wanaonisifu?
- Je, ninamtafuta Mungu kwa dhati, au ninafanya tu mambo sahihi ya nje? Njia moja ya kujua ni kumtazama mtu ambaye ni wewe ambapo hakuna anayeangalia. Unaitendeaje familia yako ambapo hakuna anayejua? Je! Umejitoleaje kwa mambo ya Mungu wakati hakuna mtu anayeangalia? Je, unapenda kweli au unapendezwa zaidi na watu wanavyokifikiria wewe ni mtakatifu?
- Je, ninaweza kumpenda jirani yangu kwa dhati, au ninahitaji kumwomba Mungu abadilishe moyo wangu ili niweze kupenda kweli?

Ombeni mmoja mmoja, wawili wawili, au kama kikundi kwamba Mungu atabadilisha mioyo yetu na matendo yetu kuonesha kweli nuru ya upendo wake kwa jamii zetu.

Masomo yetu yajayo yatatufundisha jinsi ya kukua kiroho ili mioyo yetu impendeze Mungu.

Somo la 4: Kuondoa Dhambi & Kufanya upya Akili zetu

Lengo kuu:

1. Lazima tuchukue hatua za kushinda dhambi ili tuwe kama chumvi na nuru katika jamii zetu.

Vifaa:

- Mwongozo wa Wanafunzi: Hatua za Kushinda Dhambi (pamoja na maandiko na picha)
- Vioneshi: Mchezo wa Doti nyeusi (chapisha au tengeneza kadi za kutosha ili kila mtu awe na kadi moja - kata safu ya kwanza kuonesha kikundi na ukate sehemu zingine zote nyeusi na uweke ndani ya bahasha au mfuko)
- Vioneshi: Picha sita - tatu kwa ajili ya hatua za 'Kuondoa Dhambi' na tatu za 'Kuzifanya upya Akili zetu'
- Bango la hatua 9 za Kushinda Dhambi (tengeneza au andika kwenye ubaoni) na nafasi kati ya kila hatua

Maelekezo kwa Mwalimu: *Ni muhimu kufanya mazoezi ya maonesho ya somo hili kabla ya kuyawasilisha ili uwe na hakika na ufanisi jambo linalofundishwa. Pia, michezo mikubwa ya kikundi inahitaji maandalizi kwa upande wa mwalimu, hivyo hakikisha una vifaa vyovyote kabla ya somo.*

Utangulizi: Kupoteza (ladha ya) Chumvi yako

Katika Somo la 1 tulisoma Mathayo 5:13: 'Ninyi ni chumvi ya dunia. Lakini ikiwa chumvi imeharibika, itatiwa nini hata ikolee? Haifai tena chochote, isipokuwa kutupwa nje na kukanyagwa na watu. '

Tulizungumzia juu ya thamani na umuhimu wa chumvi na jinsi maisha yetu yanapaswa kuwa kama chumvi kwa jamii zetu. Sasa tutaangalia sehemu ya pili ya kifungu hiki-kinatokea nini ikiwa chumvi inakuwa 'haina ladha ya chumvi.'

Kuondoa Dhambi

- Dhambi ni nini? *(kufanya makosa, mawazo mabaya au matendo, kumkosea Mungu)*
- Inamaanisha nini kuwa 'mwenye dhambi'? *(tunataka kutenda dhambi, tuna tabia ya kutenda dhambi, tabia yetu ya asili ni kutenda dhambi, tuna dhambi maishani mwetu*)

Dhambi hutufanya tusiwe na chumvi na tusifanikiwe katika jamii zetu. Tutacheza mchezo rahisi ili kujua ni nani kati yetu anahitaji kushinda dhambi maishani mwetu na ni yupi hana dhambi maishani mwetu.

SHUGHULI YA KIKUNDI KIKUBWA: Mchezo wa doti nyeusi

Maelekezo kwa Mwalimu: *Onesha kikundi kadi mbili za* ***VIONESHI****: moja yenye doti tupu na moja yenye doti nyeusi.*

Doti tupu inawakilisha moyo safi usio na dhambi na doti nyeusi inawakilisha moyo wenye dhambi.

Kwa kazi hii, tutatumia sehemu ya mbele ya darasa. Sasa nafasi hii imegawanywa katika sehemu mbili:

- Sehemu ya 1 - 'yenye dhambi'
- Sehemu ya 2 - 'Sio yenye dhambi'

Maelekezo ya mchezo:

1. Kila mmoja wenu atapokea kadi iliyo na doti. Kadi hiyo itaamua utaenda upande upi wa darasa: doti nyeusi = sehemu yenye 'dhambi', au doti tupu =sehemu 'isiyo na dhambi'.
2. USITAZAME doti mpaka nitakapokuelekeza kwamba ni zamu yako. Ficha kadi yako ili mtu asiweze kuona doti yako — hata wewe mwenyewe!

***Maelekezo kwa Mwalimu**: Waoneshe kadi ya **VIONESHI** iliyo na doti nyeusi na onesha kuwa kadi hii itawapeleka upande wa chumba/darasa ulichoteuliwa kuwa wenye "dhambi." Onesha kadi iliyo na doti tupu na uoneshe kuwa kadi hii itawapeleka upande wa chumba/darasa ulioteuliwa kama "sio wenye dhambi."*



- *Gawa kadi moja kwa kila mshiriki (TUMIA DOTI NYEUSI TU.)*
- *Wakumbushe wasitazame kadi zao!*
- *Mmoja mmoja, mwite kila mtu mbele na uwaambie waangalie kadi zao na kisha waoneshe darasa.*
- *Waambie wahamie upande unaofaa wa chumba na endelea kushikilia kadi yako huku ikionekana kwa wanadarasa.*
- *Baada ya kila mtu kuwa na zamu, washiriki WOTE watakuwa upande wa chumba kilichoteuliwa 'Dhambi.'*
- *Kisha soma yafuatayo:*

Kulingana na 1 Yohana 1: 8, sisi wote tuna dhambi. 'Tukisema kwamba hatuna dhambi, tunajidanganya wenyewe, na ukweli haumo ndani yetu.' Kwa kuwa wote tuna dhambi, sisi wote tunahitaji kujua jinsi ya kuondoa dhambi hiyo ili tuweze kufanywa chumvi.

TAFAKARI BINAFSI NA MAOMBI

Sasa tutumie muda kidogo kuomba huku tukiwa tumesimama. Mshukuru Mungu kwa ahadi yake ya msamaha na umwombe atupe mioyo ya utayari na maelekezo ya jinsi ya kuzishinda dhambi zetu.

Hatua za kuishinda dhambi

KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO

Kwa kuwa sisi wote hatuna chumvi, tunawezaje kufanywa chumvi tena? Je, hatufai kwa chochote ila kutupwa nje na kukanyagwa? Ingawa dhambi zetu zaweza kuwa kubwa, Biblia iko wazi kabisa kwa kutupa maagizo juu ya jinsi ya kuondoa dhambi na inatuhakikishia kwamba nguvu za Mungu zinaweza kushinda dhambi zetu zote. Nguvu zake hutufanya tuwe na chumvi tena!

Katika masomo 2 yajayo tutajifunza juu ya michakato mitatu rahisi ya kushinda dhambi maishani mwetu:

1. Kuondoa dhambi
2. Kufanya upya akili zetu, na
3. Kubadilisha baya kwa zuri

Kuondoa dhambi

***Maelekezo kwa Mwalimu:** Unapofundisha sehemu mbili zifuatazo, andika kila namba na kichwa cha habari kwenye ubao au bango. Kisha onesha picha ya **VIONESHI** ambayo inawakilisha dhana mpya. Halafu endelea kuelezea kila moja. Baada ya kuelezea kila moja, rudia hoja za awali ili watu wakumbuke hatua zote. Pia kuna ukurasa wa muhtasari (ufupisho) katika **MWONGOZO WA MWANAFUNZI** kwa hatua zote tisa na maandiko yanayohusiana.*

Sasa tunangalia hatua 3 za kuondoa dhambi.

1. **Tambua Dhambi** (Picha ya **VIIONESHI**: Mkono na doti nyeusi)
   Mwombe Mungu akuoneshe dhambi fulani maishani mwako ambayo anakutaka uifanyie kazi kuibadilisha. Inaweza kuwa kitu tunachofanya-kama kusengenya-au inaweza kuwa kitu tunachoshindwa kufanya-kama kuwapenda wake zetu kama Kristo alivyolipenda kanisa.

   Tunamwona Daudi akifanya hivi katika Zaburi 139: 23-24, isemayo: 'Ee Mungu unichunguze, uujue moyo wangu; unijaribu na uyajue mawazo yangu. Uangalie ikiwa kuna njia yoyote isiyo sahihi ndani yangu, na uniongoze katika njia ya milele.

2. **Kukiri Dhambi na Kusamehewa** (Picha ya **VIONESHI**: kiboksi chenye doti nyeusi ndani)
   Mara tu dhambi hiyo imetambuliwa, tunakiri dhambi hiyo kwa Mungu na labda kwa wengine. 1 Yohana 1: 9 inasema: 'Tukikiri dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki, naye atatusamehe dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote.' Jipe moyo — hakuna dhambi iliyo kubwa kwa Mungu! Yeye ni mwaminifu wa kusamehe dhambi zetu ZOTE.



   Ikiwa tumemkosea mtu mwingine, ni muhimu kuomba msamaha wao. Ikiwa uhusiano umeharibiwa au kuvunjwa na dhambi zetu, ni muhimu kwamba tukiri na kuomba msamaha wao ili uhusiano huo urejeshwe.

3. **Tubu** (Picha ya **VIONESHI** kiboksi chenye doti nyeusi yenye x)
   Inafaa kutubu ili kutorudia dhambi. Kutubu kunamaanisha kujitoa kwa kuacha dhambi na kuelekea mapenzi ya Mungu.

   Katika Ayubu 31: 1 tunasoma: 'Nilifanya agano na macho yangu kutomtazama msichana. Hapa tunaona kwamba Ayubu alitubu na kuweka ahadi ya kutomtazama msichana kwa tamaa. Ayubu alikuwa mtu ambaye Mungu alimwita 'asiye na lawama na mnyofu' (Ayubu 1: 8), na bado Ayubu aliona ni muhimu kuweka agano/ahadi juu ya dhambi hii. Tunatiwa moyo kwamba Mungu huwaheshimu wale wanaotamani kuishinda dhambi yao! Msifuni Mungu kwamba yeye ndiye anayetufanya tusiwe na lawama na wanyofu!

Kufanya upya Akili zetu

KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO
Sasa tuangalie hatua tatu za kufanya upya akili zetu.

4. **Sali/omba kila siku** (**VIONESHI** Picha: kusali kwa mikono)
   Hatuwezi kushinda dhambi kwa juhudi zetu wenyewe tu. Hata Mtume Paulo alisema katika Warumi 7: 19-20: 'Kwa maana lile jema nilipendalo, silitendi; bali lile baya nisilolipenda ndilo nilitendalo. Sasa nikifanya lile nisilotaka kufanya, si mimi tena ninayefanya, lakini ni dhambi inayoishi ndani yangu ndiyo inayofanya. '

   Tunahitaji msaada wa Mungu uondoe dhambi mioyo yetu. Kwa maana tunajua kuwa kila siku tutakabiliwa na majaribu, kila siku tunahitaji kujiandaa kwa kuomba msaada wa Mungu. Hii inatukumbusha juu ya kumtegemea Mungu na ahadi zetu kwake. Tunahitaji kufuata onyo la Yesu kwa mwanafunzi wake Mathayo: 'Kesheni, ombeni msije mkaingia majaribuni.' (Mathayo 26:41)

   Kuomba mara kwa mara hutuweka karibu na yule aliye na nguvu za kuzishinda dhambi zetu. Ameshashinda dhambi na kifo, hivyo tunamtumaini Mungu azishinde dhambi katika maisha yetu!

5. **Kudhibiti Mawazo Yetu** (Picha ya **VIONESHI**: kiboksi cha kufikiria chenye doti tupu)
Kila dhambi hufanywa mara mbili-mara moja akilini na mara ya pili katika tabia zetu. Kwa hiyo, kwanza tunahitaji kudhibiti mawazo yetu ili kuzuia mawazo ya dhambi yasiwe kitendo cha dhambi.

Soma mistari ifuatayo:

Warumi 12: 2: 'Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya akili zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu.

2 Wakorintho 10: 5b: '… na tukiteka nyara kila fikira ipate tumtii Kristo.'

Wafilipi 4: 8: 'Hatimaye, ndugu zangu, mambo yoyote yaliyo ya kweli, yoyote yaliyo ya staha, yoyote yaliyo ya haki, yoyote yaliyo safi, yoyote yenye kupendeza, yoyote yenye sifa njema; ukiwapo wema wowote, ikiwapo sifa nzuri yoyote, yatafakarini hayo.'

Tunafanyaje 'kuteka nyara kila fikra/wazo'? Tunapotambua fikra/wazo la dhambi (kwa mfano, kunung'unika, 'Ninafanya kazi kwa bidii na familia yangu haithamini yote ninayowafanyia.'), Tunaweza kukiri kwa Kristo mara moja na kuchagua wazo jipya (kwa mfano, ' Ninachagua kumfanyia kazi Mungu na kwa utukufu wake. Sitatarajia shukrani kutoka kwenye familia yangu, lakini nitatafuta kumpendeza Mungu na kazi yangu na mtazamo wangu. ') Yote haya yanaweza kutokea katika muda mfupi, unapoendelea na siku yako. Rudia hivi mara kwa mara fikra/mawazo ya dhambi yanapokujia-Mungu hachoki kutusamehe na kutusaidia.

6. **Kariri maandiko** (**VIONESHI** Picha: Kiboksi cha kufikiria chenye kitabu wazi ndani yake)
Kukariri maandiko hutusaidia kudhibiti mawazo yetu na kuweka ukweli kila wakati kwenye akili zetu. Kila tunapoanza kufikiria mawazo mabaya, badala yake, tunaweza kusoma mistari ambayo tumekariri kujaza akili zetu kwa ukweli. Kwa njia hii, 'tunafanya upya akili zetu' kwa kuondoa yaliyo mabaya na kuyaweka yaliyo mema.



Yesu alipoenda jangwani na Shetani alikuja kumjaribu, Yesu alinukuu maandiko ili kushinda majaribu ya Shetani ya kutenda dhambi. Zaburi 119: 11 inasema, 'Moyoni mwangu nimeliweka neno lako, nisije nikakutenda dhambi.'

Biblia imeweka wazi kwamba kukariri maandiko hutusaidia kushinda dhambi. Daima tunaweza kupata sehemu inayofaa ya maandiko inayohusiana na dhambi tunayojaribu kuishinda. Ikiwa hujui wapi unaweza kupata andiko, mwulize mchungaji au rafiki mwingine anayeweza kukuelekeza. Kariri maandiko, na yatakusaidia kulishinda jaribu linapotokea.

SHUGHULI YA KIKUNDI KIKUBWA

Maelekezo kwa Mwalimu: *Shikilia picha na uwaambie wanadarasa wasema hatua ya picha hiyo. Kwa mfano, shikilia picha ya mkono iliyo na doti nyeusi na washiriki waseme kwa sauti, "Tambua dhambi!" Unaweza kuweka alama ukitaka kuleta ushindani: mtu wa kwanza kusema hatua ya picha anapata alama/pointi!*

Hitimisho

Sisi wote tuna dhambi mioyoni mwetu. Hakuna hata mmoja wetu asiye na lawama na safi. Uchafu wa dhambi zetu ni kama uchafu tulioona kwenye chumvi: dhambi huondoa chumvi yetu. Mungu anatamani kusamehe matendo yetu ya dhambi na kutusaidia kuondoa dhambi hiyo maishani mwetu. Kuondoa dhambi kwenye

maisha yetu kunatufanya tuwe na chumvi tena na kunatuwezesha kuwa na ufanisi zaidi katika kufanya Matendo ya Upendo katika jamii zetu.

Kushinda dhambi kwenye maisha yetu kunahitaji mazoezi na kazi. Tumeona leo kwamba kushinda dhambi kunatokea kwanza kwa kuondoa dhambi na halafu kuzifanya upya akili zetu. Hii ni michakato inayotumia muda, lakini usivunjike moyo. Yesu tayari ameshinda dhambi na kifo! Nguvu zake zinaweza kushinda dhambi katika maisha yetu, pia.

Maelekezo kwa Mwalimu: *Unapomaliza somo, mwombe mtu aombe kwamba Mungu atawasaidia wanadarasa/wanafunzi kuondoa dhambi ambazo anawafunulia kwamba anataka kuwasaidia kuzishinda. Hasa omba kwamba neno lake na maisha yake yatabadilisha upya akili zetu zote kwa kujazwa ukweli na upendo wake.*

Somo la 5: Kubadilisha Baya kwa Zuri.

Malengo makuu:

- Kubadilisha tabia mbaya kwa tabia njema ni muhimu kushinda dhambi katika maisha yetu.
- Lazima tuchukue hatua kushinda dhambi ili tuwe kama chumvi na nuru katika jamii zetu.

Vifaa:

- Mwongozo wa Mwanafunzi: Jedwali la Kushinda Dhambi - mfano wa kulalamika na jedwali tupu (toa nakala 1 kwa kila mtu / kikundi). Karatasi hii ya kazi pia inapatikana mwishoni mwa Mwongozo huu wa Mwalimu.
- Vioneshi: Picha za hatua za 6-9 za Kushinda Dhambi (jumla 3).

Utangulizi

Katika somo la mwisho, tulicheza mchezo wa kutukumbusha kwamba sisi WOTE tuna dhambi mioyoni mwetu. Tuliona kwamba lazima tuishinde dhambi kwa kuondoa na kufanya upya akili zetu. Sasa tutaangalia jinsi ya kubadilisha tabia mbaya za njia zetu za dhambi.

SHUGHULI YA KIKUNDI KIKUBWA

Maelekezo kwa Mwalimu: *Hadithi hii inaweza kusomwa kwa sauti, au kuigizwa na washiriki/wanafunzi kwa ukimya huku ukiwa unaisoma hadithi.*

Sikiliza hadithi hii…

Kulikuwepo na mwanaume aliyekuwa akijenga nyumba. kila alipopata pesa za kutosha, alikuwa akizitumia kujenga nyumba kidogo kidogo kwa wakati. Mara baada ya nyumba hiyo kukamilika, alipanga kuihamishia familia yake kwenye nyumba hiyo. Oh, jinsi alivyoitarajia siku hiyo! Kulikuwa na shida moja tu: kwa kuwa aliishi mbali, hakuwa karibu kuisimamia nyumba mpya kila siku. Hii ilileta shida kwa mwanaume huyo.

Mwanzoni, kuta zilipokuwa bado hazijamalizika, wakati mwingine alikuwa akija nyumbani na kukuta kwamba mbuzi na kuku wa jirani walikuwa wanakula nje na ndani ya nyumba. Hili halikuwa tatizo kubwa, lakini lilileta uchafu. Mwanaume huyo alikamilisha kuta na kuzuia mlango ili wanyama wasiweze kuingia tena.

Wiki kadhaa baadaye, alikuja kufanya kazi kwenye nyumba hiyo na kugundua kwamba panya walikuwa wamezaliana kwenye kona. Aliondoa nyumba ya panya na kumalizia ujenzi wa paa la nyumba, akitumaini paa hilo litawazuia panya wasiingie.

Wakati mwingine, alifika nyumbani hapo na kugundua kwamba kundi la popo lilikuwa limekaa kwenye paa jipya la nyumba hiyo! Aliwaondoa popo na kuziba sehemu zilizo wazi kwa wavu.

Tena, alikuja nyumbani na kuona kwamba jirani mwingine alikuwa ametumia nyumba hiyo kuanzisha biashara yake ndogo ya kuwauzia pombe za kienyeji wanaume wa kijiji. Alikasirika kwa kuwa nyumba yake inatumiwa bila ruhusa yake, alimtaka mwanamke huyo ahamishe biashara yake. Alifunga mlango kwa kufuli na kuondoka.

Miezi kadhaa akapita. Kwa mara nyingine, mwanaume huyo alikuja katika nyumba na kuona kufuli limevunjwa na mlango ulikuwa ukining'inia. Mgeni alikuwa ameifanya nyumba hiyo kuwa mahali pake pa kupumzikia. Mwanaume mwenye vurugu na mlevi, alikuwa ameharibu mwonekano wa ndani ya nyumba na

kutishia kumpiga mwenye nyumba. Mwenye nyumba alilazimika kuihusisha mamlaka ya serikali za mitaa ili mtu huyo aondolewe.

Mwishowe, mwanaume huyo aligundua kwamba, kadiri ambavyo nyumba yake ingeachwa tupu, kitu fulani kingeingia humo. Bila kuchagua kitu gani kikae humo, bila shaka wadudu wasiokubalika na watu wasiokuwa na faida yoyote wangeingia katika nyumba hiyo. Aliamua lazima achague wapangaji wake mwenyewe: wanandoa watulivu watakaoitunza nyumba ndogo na kuitunza vizuri hadi familia yake itakapoweza kuhamia.

Miezi ilipita na yule mwanaume alirudi kukamilisha hatua za mwisho za maandalizi ya nyumba hiyo. Alifurahi kuona kwamba wanandoa hao walikuwa wameitunza nyumba hiyo katika hali nzuri! Mlango ulikuwa salama kwenye bawaba zake, madirisha yalikuwa yamewekewa mapazia mazuri kuzuia vumbi, ndani hamkuwa na wadudu, na hata uwanja ulifagiliwa!

- Nyumba ilipoachwa tupu kilitokea nini?
- Je, mwenye nyumba alifanya nini kuzuia wadudu wasiohitajika na watu?
- Tunajifunza nini kwenye hadithi hii?

Mwanaume katika hadithi hii aliendelea kuwaondoa wadudu na akaikarabati nyumba yake kwa kusafisha baada ya kuwaondoa wadudu na kuwazuia wasirudi, lakini kila mara aliporudi, alimkuta mdudu mwingine! Alihitaji kukamilisha hatua ya mwisho ya kuwashinda wadudu, ambayo ilikuwa kupangisha nyumba kwa busara kwa hiyo, wadudu waliondoka, na nyumba ilikaliwa na wapangaji wazuri.

Mioyo na akili zetu ni kama nyumba ya mwanaume huyu. Mara nyingi tunashinda eneo moja la dhambi na kuona kwamba jaribu jipya limejitokeza. Kama yule mwanaume katika hadithi, tunahitaji kumaliza mchakato wa kushinda dhambi maishani mwetu kwa kubadilisha tabia mbaya kwa tabia nzuri. Kujaza mioyo na akili zetu kwa ukweli na upendo wa Mungu ni kinga bora dhidi ya dhambi kuja kuishi mioyoni mwetu tena.

Tujifunze juu ya hatua 3 za mwisho za kushinda dhambi.

Maelekezo kwa Mwalimu: *Rudia kwa haraka hatua 6 ulizofundisha katika somo lililopita. Fundisha hoja zifuatazo kwa njia ile ile uliyofanya katika hatua 6 za kwanza: andika hatua kwenye bango na utambulishe kila picha kabla ya kuendelea na hoja inayofuata.*

Kubadilisha Baya kwa Zuri

KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO

7. **Kukimbia majaribu** (Picha ya **VIONESHI** :mtu anayekimbia doti nyeusi)
   Kushinda dhambi ni kama vita/mapigano. Katika vita, unahitaji kumjua adui yako. Kushinda dhambi sio tofauti. Tunapaswa kujijua wenyewe na udhaifu wetu. Yakobo 4: 7 inasema, ***"Basi mtiini Mungu. Mpingeni shetani, naye atawakimbia."***

   Epuka majaribu. Ikiwa una shida na kunywa pombe usiende kwenye baa ili ushirikiane na rafiki zako. Ikiwa tatizo lako ni la wivu basi epuka vitu vinavyokufanya uwe na wivu mpaka uweze kujifunza kutosheka na yale yote ambayo Mungu amekupa. Utiwe moyo na maneno haya kutoka 1 Wakorintho 10:13: *'Jaribu halikuwapata ninyi, isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu; ila Mungu ni mwaminifu; ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo; lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlango wa kutokea, ili mweze kustahimili.'*

8. **Kuza tabia mpya** (Picha ya **VIONESHI** : mtu aliye na doti nyeusi akibadilishwa na doti tupu / isiyo nyeusi)

Katika nafasi ya tabia zetu za zamani za dhambi, tunahitaji kuanza kukuza tabia mpya. Kwa mfano, ikiwa nitatubu kwa kukasirika niliporudi nyumbani na kukuta kwamba mke wangu hajaandaa chakula, ninaweza kutengeneza tabia ya kuuliza ni namna gani tunaweza kusaidia kumaliza kazi na kutafuta njia za kumsaidia. Nikiwa nimeamua kuacha kukutana na marafiki baa kila jioni, ninaweza kufanya mazoea ya kutumia muda huo ya kuwa na watoto wangu. Ikiwa nina shida ya kulalamika au kuwa na kinyongo, ninaweza kukuza tabia kila jioni ya kutaja vitu vitatu ninavyoshukuru kwa siku hiyo.



9. **Uwajibikaji** (**VIONESHI** Picha: watu wawili wanasaidiana wakiwa na doti nyeupe vifuani)
Hii ni muhimu kwa mafanikio katika kushinda dhambi!



Tunapofanya uchaguzi mzuri na kukuza tabia nzuri ya kuepuka dhambi, itakuwa rahisi kushinda dhambi wakati ujao. Kila mara tunapofanya chaguo sahihi, inakuwa rahisi kidogo. Kuanzisha tabia ya kufanya chaguo sahihi ni rahisi ikiwa utafanya pamoja na mtu atakayekusaidia na kukutia moyo. Tafuta mtu atakayekuwajibisha kufikia tabia yako nzuri na atakuhimiza au kukutia moyo na kukuthibitisha unapofanya uchaguzi mzuri katika eneo hilo.

Kwa kuwa kushinda dhambi ni vigumu, tunahitaji rafiki mmoja au wawili ambao wanaweza kutusaidia katika mapambano. Marafiki hao wanapaswa kuwa waumini ambao pia wanashiriki kujitolea kwetu kwa mafunzo katika utakatifu. Wao, pia, wanapaswa kufanya kazi ya kushinda dhambi maishani mwao na wanapaswa kuwa tayari kukushirikisha juu ya shida zao.

TAFAKARI BINAFSI
Soma Mhubiri 4: 9-10.

> ‘Afadhali kuwa wawili kuliko mmoja; kwa sababu wana faida nzuri kwa kazi yao. Kwa maana wakianguka, mmoja wao atamwinua mwenzake; lakini ole wake aliye peke yake aangukapo,wala hana mwingine wa kumwinua!. '

- Omba na umwombe Mungu akuoneshe ni nani unayeweza kukutana naye mara kwa mara kwa ajili ya maombi na kutiana moyo wakati wote mnafanya kazi ya kuzishinda dhambi na majaribu.

SHUGHULI YA KIKUNDI (Hiari): *Ikiwa kundi lako linajua kusoma na kuandika na kutumia biblia, unaweza kuunda vikundi vidogo na kutafuta mistari ifuatayo ambayo inajibu swali: 'Ni njia gani ambazo tunaweza kusaidiana katika vita dhidi ya dhambi?'*

- Wakolosai 3:16 - *kufundishana na kuonyana*
- Waebrania 3:13 - *kuhimiza*
- Yakobo 5:16 - *kukiri na kuomba*
- Wagalatia 6: 2 - *kubebeana mizigo*
- Waefeso 4:29 - *jenganeni kulingana na mahitaji yao*

Kujizoeza Kushinda Dhambi

SHUGHULI YA KIKUNDI KIDOGO
Maelekezo kwa Mwalimu: *Onesha kwa kikundi/darasa jinsi kila hatua 9 inavyoweza kutumika kushinda dhambi fulani (kulalamika ni mfano uliooneshwa kwenye jedwali la mfano mwishoni mwa somo hili).*

- Ni dhambi gani 4-5 za kawaida katika eneo hili?

Maelekezo kwa Mwalimu: *Baada ya kundi/darasa kubainisha dhambi 4-5 zilizo za kawaida katika eneo hilo, basi wagawanyike katika vikundi na kila kikundi kipewe moja ya dhambi hizo kujadili. Vikundi viongee kwa kuangalia kila hatua ya dhambi hiyo. Kisha kikundi kimoja kiwasilishe jinsi walivyopitia kila hatua kwa dhambi yao waliyopewa.*

- Tumia jedwali la **MWONGOZO WAKO WA MWANAFUNZI** kufikiria ni jinsi gani unaweza kutumia kila moja ya hatua hizo 9 kushinda moja ya dhambi za kawaida zilizotajwa.

TOA RIPOTI

Hitimisho

TAFAKARI BINAFSI
Omba na umwombe Mungu akuoneshe dhambi ambayo anataka uishinde. Tumia muda mfupi kusikiliza kwa utulivu ili alete kitu akilini mwako. Halafu umwombe akusaidie kufuata hatua za kuishinda.

KUSHINDA DHAMBI

JEDWALI LA MFANO – Kulalamika

HATUA	PICHA	DHAMBI
KUONDOA DHAMBI		
1. Tambua dhambi		Kulalamika
2. Kiri & usamehewe		Ninakiri kwamba nalalamika juu ya kufanya kazi kwa nguvu sana. Tafadhali nisamehe kwa kulalamika.
3. Tubu		Siutaki moyo unaolalamika. Badala ya kulalamika, nataka kusema mema na kushukuru kwa kile nilicho nacho.
KUFANYA UPYA AKILI ZETU		
4. Omba kila siku		Ninahitaji msaada leo wa kutolalamika. Tafadhali nisaidie niwe mwenye kushukuru na kufanya kazi kwa furaha.
5. Kudhiti akili zetu		Ninapolalamika, ninajifikiria mwenyewe tu. Badala yake, nataka kufikiria jinsi kazi iliyo mbele yangu inavyoweza kutumika kumtukuza Mungu. Ninataka kumfikiria yeye badala ya mimi mwenyewe.

6. Kariri maandiko		Waefeso 4:29 inasema: 'Neno lolote lililo ovu lisitoke vinywani mwenu, bali lililo jema la kumfaa mwenye kuhitaji, ili liwape neema wanaosikia.'
BADILISHA BAYA KWA ZURI		
7. Kukimbia majaribu		Mimi hulalamika kila ninapokuwa na _____. Nahitaji kutotumia muda pamoja naye au kumwambia kwamba sitaki kulalamika tena.
8. Kuza tabia mpya		Ninapojaribiwa kulalamika, nitafikiria vitu 3 ninavyoshukuru. Nitamshukuru Mungu kwamba anaweza kutumia hali hiyo kumletea utukufu.
9. Uwajibikaji		Nitamwambia ____ juu ya hamu yangu ya kuacha kulalamika. Nitamwomba aniwajibishe, na atakapouliza juu ya hili, sitajaribu kuficha dhambi zangu au kujifanya nionekane bora. Nitajitahidi pia kumsaidia _____ kushinda dhambi ikiwa ataniruhusu nimwajibishe.

Somo la 6: Namna ya kuwa Kanisa la Chumvi na Nuru

Malengo makuu:

1. Makanisa yetu yanaamriwa kuwa chumvi na nuru au mwanga kwa jamii zetu.
2. Kwa nguvu ya Mungu kanisa lenye chumvi na nuru linaweza kubadilisha jamii yao.

Vifaa:

- Karatasi au ubao na makapeni.

Kwa nini tushiriki katika kuwahudumia wengine?

Katika masomo haya 3 yajayo tutaangalia jinsi tunavyoweza kuwa kanisa lenye chumvi na nuru kwa jamii yetu.

KIKUNDI KIDOGO CHA MAJADILIANO

Katika vikundi vidogo fikiria sababu nyingi iwezekanavyo kwa nini Wakristo na kanisa wanapaswa kushiriki kuwahudumia maskini. Jaribu kufikiria kutoka masomo yote ambayo umejifunza tangu Moduli 1 hadi sasa. Ikiwezekana, jaribu kukumbuka mistari fulani ya biblia.

TOA RIPOTI

Notsi za Mwalimu: *Mara vikundi vinapomaliza kushirikisha maelezo yao, ongezea hoja yoyote kati ya hizi ambazo zimekosekana.*

- *Mungu alimtuma Yesu afe ili apatanishe mahusiano 3 yaliyovunjika Adamu alipotenda dhambi. Uhusiano wetu na Mungu, uhusiano wetu baina ya wanadamu, na uhusiano wetu na uumbaji. Tumeitwa kwenye huduma hiyo ya upatanisho — kuleta uponyaji kwa mahusiano yote 3.*
- *Watu ni wa muhimu kwa Mungu — kiasi kwamba alimtuma mwanawe alikufa kwa ajili yao. Ikiwa Mungu anafikiria kuwa watu ni wa muhimu sana kwamba angekufa kwa ajili yao basi sisi pia tunapaswa kuwajali watu.*
- *Katika Isaya 58 Mungu alisema kwamba hakujibu maombi ya kanisa kwa sababu walishindwa kuwajali wajane na yatima.*
- *Yesu au Paulo walipofupisha Agano la Kale, mara 3 walifanya hivyo kwa mafundisho kwamba tunapaswa kumpenda Mungu na kumpenda jirani yetu. Mara tatu juu ya mafundisho kwamba tunapaswa kumpenda jirani yetu. Ingawa kumpenda Mungu ni muhimu zaidi, lakini Biblia inasema mara tatu tuwapende jirani zetu — kwa sababu hivyo ndivyo tunavyoonesha upendo kwa Mungu.*
- *Katika mfano wa Msamaria Mwema, Msamaria Mwema alimtunza yule mtu aliyepigwa na kumpatia mahitaji; wala hakumhubiria.*
- *Katika mafundisho juu ya kondoo na mbuzi, Yesu alifundisha kwamba tuwape chakula wenye njaa, maji wenye kiu, kuwatembelea wagonjwa au wafungwa, na kuwavika walio uchi. Tunapomfanyia mtu mwingine, ni kana kwamba tunamfanyia Kristo.*
- *Tumeitwa kujenga ufalme wa Mungu. Inamaanisha tunataka watu zaidi wawe Wakristo na tunataka Wakristo wazidi kumtii Mungu katika kila eneo la maisha yao.*
- *Mungu ameahidi kwamba, tukimtii, atatubariki. Ametupa miongozo ya kuifuata itakayotusaidia kuboresha maisha yetu. Tunahitaji kuwa watiifu kwake.*

Tumia muda kufikiria:

- Je, unaamini kwamba ni sharti na jukumu la kanisa kuwajali maskini na kuonesha upendo kwa jamii zao?

Ni muhimu kuamini kwamba kuwajali maskini na kubadilisha jamii zetu sio jambo la hiari. Ni sehemu ya maana ya kuwa Mkristo na njia ambayo tunaonesha upendo wetu kwa Mungu.

Kijiji kimebadilishwa

KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO

Kama tulivyoona, ni muhimu tufuate amri ya Mungu ya kumpenda jirani yetu. Sikiliza hadithi ya kanisa hili ambalo lilitumia masomo ya TCT ambayo umekuwa ukijifunza. Tumia muda kufikiria juu ya kile walichofanya na matokeo yalikuwaje.

HADITHI YA KWELI – Kijiji kimebadilishwa

Kuna kijiji katika eneo la mbali. Kipo mbali milimani na ni kijiji rahisi sana. Watu katika kijiji hicho walikuwa wakitengeneza mvinyo wa mchele na wanalima na kuvuta tumbaku. Walifanya kazi mara chache, lakini mara nyingi walikuwa wakilewa mvinyo wa mchele waliotengeneza. Usafi katika kijiji ulikuwa mbaya sana; walioga mara moja kwa mwezi, walinawa mikono mara chache, na hawakuwa na vyoo. Mavazi yao yalikuwa chakavu, na watoto walivaa kidogo sana.

Kiuchumi, kijiji kilipata shida. Hakukuwa na barabara halisi kati yao na barabara kuu — ilikuwepo njia tu ya kutembea. Kwa sababu ya hii, watu wangeweza kuuza tu mavuno yao kadri walivyoweza kubeba kwenye migongo yao safari ndefu hadi sokoni. Kwa kuwa hawakuweza kuuza zaidi, walifanya juhudi kidogo kupanda mazao mengi katika mashamba yao.

Watu katika kijiji hicho walikuwa Wakristo, lakini hawakuwa wamejifunza sana kuhusu Mungu. Hawakuwa na kiongozi wa kanisa, na hakuna wachungaji wangeenda katika eneo hilo kwa sababu barabara zilikuwa hazipitiki. Ili kutembelea ulilazimika kuacha pikipiki yako kwenye barabara kuu na utembee kwa masaa 3, ukitumaini kwamba unaporudi pikipiki utaikuta haijaibiwa! Hawakuwa na mahali pa mkutano, na hawakuwa wakikua kiroho kabisa.

Kanisa lilisikia juu ya programu ya TCT na likamsihi kiongozi katika eneo lao awajumuishe kwenye mafunzo. Kwa muda mrefu hakuna mwalimu aliyetaka kwenda — ilikuwa safari ndefu na ngumu. Na hata walipokuwa wametembea kwenda kijijini, hali ya usafi ilikuwa chini sana hivyo walikuwa na hakika kwamba watapata magonjwa. Lakini, Mungu alizungumza na mmoja wa wakufunzi/walimu na mwishowe alikubali kwenda.

Kanisa lilianza kusoma programu ya TCT. Moja ya miradi ya kwanza ambayo Mungu aliwapa changamoto ya kuifanya ilikuwa kupanua njia ya kutembea kutoka kijiji chao hadi barabara kuu — umbali wa kilomita 10 kupitia milima. Walimtii Mungu na kupanua barabara kwa kutumia zana za mikono. Ilikuwa kazi ngumu sana, lakini Mungu aliwabariki. Matokeo ya barabara hii bei zao za mazao ziliongezeka kwa sababu waliweza kupeleka mazao sokoni kwa haraka sana huku yakiwa katika ubora. Barabara kubwa ilimaanisha kwamba wangeweza pia kuuza zaidi — hawakuhitaji tena kubeba mazao yao mgongoni. Kwa sababu sasa wangeweza kupata faida nzuri, walihamasika kufanya kazi kwa bidii na kunywa kidogo. Watu walianza kufanya kazi zaidi katika mashamba yao, walizalisha na kuuza mara kumi ya kiwango walichokuwa wakipata zamani!

Kijiji hicho si moja wapo ya kijiji chenye maendeleo duni zaidi, lakini kinaendelea haraka. Kwa sababu kanisa lilitumia masomo ya afya na kufundisha katika jamii, kila mtu anajua jinsi ya kutibu magonjwa ya kawaida, na kila mtu ana choo, na bustani ya mboga. Kanisa lilianzisha mpango wa kusoma na kuandika; kwa kuona ari yao

ya kujifunza, serikali ilijenga shule. Pia, Mungu amewabarikia umeme licha ya ukweli kwamba vijiji vingi kati yao na vijiji vilivyo karibu na usambazaji wa umeme bado havina umeme.

Kijiji hiki ni mfano kwa watu wengi wanaowazunguka jinsi Mungu anavyoleta baraka wakati watu wake wanapotii kwa uaminifu amri yake ya kuwapenda wengine. Baada ya miaka mitatu walipoulizwa walikuwa wamefanya Matendo ya Upendo mangapi, hawakuweza kutoa idadi. Hata walipoulizwa katika miezi mitatu iliyopita walifanya matendo ya upendo mangapi, yalikuwa mengi mno kuorodhesha. Badala yake walieleza kuwa hufanya Matendo ya Upendo moja au mawili kwa wiki na sasa ni sehemu ya maisha yao. Wakiona kitu kinachohitajika kufanywa, basi wanakwenda kufanya kitu hicho!

- Je, matokeo ya Matendo ya Upendo katika kijiji hiki yalikuwa yapi?
- Imewezekanaje kanisa moja, lenye maarifa kidogo kuhusu Mungu, limeweza kubadilisha kijiji chao chote?
    - *Walifanya kile* ambacho *Mungu aliwaonesha wafanye.*
    - *Walikuwa na bidii ya kutumia yale waliyojifunza.*
- Ni kwa namna gani kanisa hili linaweza kutumika kama hamasa kwa kanisa lako?

Jinsi ya kuleta mabadiliko

KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO

Makanisa ambayo yameona mabadiliko makubwa sana katika jamii zao ni makanisa ambayo yamejitolea kufanya kila aina ya Matendo ya Upendo — makubwa na madogo — na kuyafanya mara kwa mara, kama kila mwezi au hata kila wiki mbili!

Hebu tuangalie njia 4 ambazo sisi kama kanisa tunaweza kusaidia kuleta mabadiliko kwenye jamii zetu.
Maelekezo kwa Mwalimu: *Andika aina 4 za Matendo ya Upendo ubaoni au tengeneza bango na waalike wengine wasome.*

1. **Matendo ya Upendo ya mtu binafsi** - Mtu mmoja anahudumia familia yake na majirani.
2. **Matendo ya Upendo ya kanisa au kikundi kidogo** - Waumini washiriki katika mradi ambao unatumia siku moja au mbili kukamilika.
3. **Matendo makubwa ya Upendo** - Shughuli kubwa zinazotumia zaidi ya siku mbili na mara nyingi huhusisha wanajamii kutoka nje ya kanisa. (kwa mfano: kujenga barabara)
4. **Elimu endelevu** - Kuwafundisha wengine masomo ya TCT.

SHUGHULI YA KIKUNDI KIDOGO

- Kanisa lako limeshakuwa linafanya nini kuhudumia jamii kwa kila njia hizo?
- Umeona matokeo gani katika jamii?
- Umeonaje Mungu akibariki au kuzidisha juhudi zako?

TOA RIPOTI

- *Baada ya kumaliza, alika vikundi vidogo kuwasilisha shuhuda zao kwa kundi kubwa/darasa.*

Hitimisho

Leo tunapomaliza leo tunataka kutumia muda kumshukuru Mungu kwa kutusaidia kufikia kile ambacho kimefanyika na kwa matokeo kutokana na matendo yetu. Tumia muda kumshukuru Mungu, chagua nyimbo kadhaa za ibada/kuabudu au zozote zinazofaa kusherehekea katika kanisa lako.

Somo la 7: Hatua zinazofuata

Malengo makuu:

1. Tunahitaji Matendo ya Upendo mbalimbali tukitaka kuona jamii yetu inabadilika.
2. Maombi ni sehemu muhimu ya mchakato wa kupanga Matendo ya Upendo.

Vifaa:

- Mwongozo wa Mwanafunzi: Hatua za Kupanga Matendo ya Upendo
- Bango la aina za Matendo ya Upendo (ama tengeneza bango au andika ubaoni)
- Bango la mafundisho yanayoendelea / endelevu (ama tengeneza bango au andika ubaoni)

Marudio

KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO

Nani anayeweza kukumbuka njia nne za kuleta mabadiliko ambazo tuliangalia katika somo lililopita?

1. **Matendo ya Upendo ya mtu binafsi** - Mtu mmoja anahudumia familia yake na majirani.
2. **Matendo ya Upendo ya kanisa au kikundi kidogo** – Waumini wanashiriki katika mradi ambao unatumia siku moja au mbili kukamilika.
3. **Matendo makubwa ya Upendo** - Shughuli kubwa ambazo zinztumia zaidi ya siku mbili na mara nyingi huhusisha wanajamii kutoka nje ya kanisa. (kwa mfano: kujenga barabara)
4. **Elimu endelevu** - Kuwafundisha wengine masomo ya TCT.

Leo tutaangalia ambacho tunaweza kufanya ili kutekeleza haya katika kanisa letu.

Maeneo manne

Soma Luka 2:52.

- Je, kuna mtu yeyote anayeweza kukumbuka ni maeneo yapi ambayo Yesu alikulia?
    - Hekima, Kimwili (kimo), Kiroho (akimpendeza Mungu), Kijamii (akiwapendeza wanadamu)
- Ni mifano gani ya mahitaji ambayo iko katika kila moja ya makundi haya?
    - *Hekima - elimu, ujuzi wa kujifunza kama vile jinsi ya kutibu magonjwa au kusimamia pesa*
    - *Kimwili - afya, nyumba imara, usalama wa chakula, maji safi*
    - *Kiroho - wokovu, kuwa karibu na Mungu*
    - *Kijamii - mahusiano ya ndoa na uzazi, mahusiano ya kijamii*

Maelekezo kwa Mwalimu: *Andika maeneo hayo manne ubaoni au rudia kusema pamoja na wanafunzi mara kadhaa hadi kikundi kizima kikariri orodha hiyo.*

Haya ni maeneo manne ambayo Yesu alikua na pia yanaunda mfano wa jinsi familia zetu, jamii zetu na sisi wenyewe tunavyopaswa kukua. Wakati mwingine inawezekana kukwama katika kufanya aina moja ya Tendo la Upendo-kwa mfano kukidhi mahitaji ya mwili au kukidhi mahitaji ya kiroho tu. Lakini tukitaka kuona jamii yetu inabadilika, basi tunahitaji kushughulikia mahitaji katika maeneo 4 yote.

KIKUNDI KIDOGO CHA MAJADILIANO

Maelekezo kwa Mwalimu: *Gawanya vikundi vidogo. Kila kikundi kipe maeneo mawili kutoka Luka 2: 52 — nusu ya vikundi vipate hekima na kimwili, nusu nyingine kiroho na kijamii. Jadili maswali yafuatayo kwa maeneo yote mawili ambayo wamepewa. Unaporipoti, anza kupitia eneo moja baada ya lingine.*

- Mambo gani ambayo kanisa tayari limefanya kuhudumia katika eneo hili?
- Mahitaji gani ambayo tuyanajua kwenye eneo hili katika jamii yetu?
- Mawazo gani ya Matendo ya Upendo ambayo tunaweza kuyafanya kushughulikia mahitaji haya?

TOA RIPOTI

Mafundisho Endelevu

KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO
Aina nne za Matendo ya Upendo kutoka kwenye orodha yetu ni 'Elimu inayoendelea/endelevu.' Elimu endelevu ni mazoezi mazuri tukiwa kanisa la chumvi na nuru. Hueneza maarifa yetu kwa wale wanaotuzunguka ili watu zaidi waweze kuishi kama Mungu anavyokusudia.

Kuna njia kadhaa tunazoweza kufundisha kwa njia endeevu/ inayoendelea.
Maelekezo kwa Mwalimu: *kwa makundi yanayoweza kusoma, andika haya ubaoni au tengeneza bango na uwaambie wengine wasome.*

1. **Mahubiri na mafundisho kutoka kwa Mchungaji** – Kwa kawaida Wachungaji ni waalimu wanaoheshimiwa kanisani na kwenye jamii. Mbali na kuleta mafundisho ya kiroho na kutia moyo kanisa, yawezekana kuwa na fursa za kufundisha juu ya ujuzi kama vile jinsi ya kuimarisha ndoa au uzazi. Hii inaweza kufanywa ama wakati wa mahubiri au wakati tofauti baada ya mahubiri.
2. **Vikundi vidogo vya kusoma** - Kusoma katika vikundi vidogo kunatusaidia kukua kiroho, kuwajibika kwa kila mmoja kwa kufanya Matendo ya Upendo ya mtu binafsi, na kuwatumikia jirani zetu pamoja kama kikundi. Vikundi vidogo pia ni vizuri kwa kufanya marudio ya masomo ambayo umejifunza katika moduli au kuwafundisha wengine ambao hawakuwepo darasani. Kila mtu kutoka kwenye vikundi vya wanawake hadi vikundi vya vijana anaweza kufaidika kwa kusikia masomo haya.
3. **Madarasa rasmi kwa wanajamii wote** - Unaweza kutumia masomo katika moduli za Afya, Ndoa & Familia, na Usimamizi wa fedha ili yaweze kufundishwa baada ya ibada au wakati wa wiki. Hii inawaruhusu Wakristo na wasio Wakristo kujifunza pamoja, kujenga uhusiano na kufungua milango ya ushirikiano.
4. **Fursa za kufundisha zisizo rasmi** - Tunapoendelea na maisha yetu ya kila siku — kuwatembelea wagonjwa, kufanya kazi shambani, kuwatunza watoto wetu, kunywa chai na rafiki — tunaweza kushirikisha kile tunachojifunza kwa wale wanaotuzunguka. Mfano mmoja ni muumini ambaye hushirikisha somo wakati wa chakula cha mchana kila wiki kwa watu anaofanya nao kazi shambani. Njia nzuri ya kuhamasisha ufundishaji usio rasmi ni kurudia kufundisha somo hilo moja kila wiki kanisani ili watu walikumbuke na waweze kuwafundisha wale wanaokutana nao katika wiki.

TAFAKARI BINAFSI NA MAOMBI
Tumia muda kuomba na kumwuliza Mungu maswali haya. Kumbuka kumsikiliza kwa utulivu ili akuoneshe ukweli na kukupa mawazo mapya.

- Tunawafundisha wengine yale ambayo tumejifunza mara ngapi?
- Tunawezaje kuongeza fursa za kufundisha? Je, kuna fursa za kufundisha ambazo hatujaona?
- Mungu ametupa rasilimali gani kwa ajili ya kufundishia? Tunakosa nini?

TOA RIPOTI
Maelekezo kwa Mwalimu: *Shirikisha mawazo. Waalike washiriki watiane moyo kwa kushirikishana jinsi ambavyo wameona mafundisho endelevu au yanayoendelea yakifanyika. Pia wakaribishe washiriki waseme ni maeneo gani ambayo bado hawako vizuri. Watie moyo kuhusu ukuaji katika maeneo hayo.*

Mchakato wa Kupanga

SHUGHULI KATIKA KIKUNDI KIKUBWA

Maelekezo ya Shughuli:

1. Ninasoma hatua za kupanga Matendo ya Upendo.
2. Kila mtu anayeweza, tafadhali usimame.
3. Kila unaponisikia ninasema neno 'omba,' upige magoti na ukunje mikono yako, kisha simama wima tena.
4. Tufanye mazoezi kwa pamoja.

Maelekezo kwa Mwalimu: *Soma* ***maneno yaliyokolezwa wino****, ukisisitiza neno "omba" kila mara unapolisoma (Kwa mfano: 'Namba 1: Kutaneni mara kwa mara… Namba 2: Ombeni pamoja… Namba 3: Tathmini mahitaji na uombe…'); darasa linapiga magoti kila wakati. Rudia hii mara ya pili (au hata ya tatu!), pitia kila hoja, kila mara kwa haraka. Mwishowe, kikundi kitakuwa kikisimama na kupiga magoti au kukaa katika maombi.*

- Kiini cha kupanga ni nini?
    - *Kuomba!*

Sasa unaweza kukaa tunaposoma kila moja ya hoja hizi. (Hamasisha kila mtu aseme maneno yaliyokolezwa wino kwa pamoja.. Kisha waombe waliojitolea kusoma kila hatua ya kupanga Matendo ya Upendo katika ***MWONGOZO WA MWANAFUNZI****, ukisoma maelezo pia; au, ikiwa haitumii Mwongozo wa Mwanafunzi, basi usome na uwaambie warudie mawazo/hoja kuu.)*

1. **Kutaneni mara kwa mara** - Kama kanisa, mnahitaji mkutane mara kwa mara ili kuzingatia Matendo ya Upendo ili watu wasije wakasahau. Mjaribu kukutana angalau mara moja kwa mwezi kuomba, kujadili Matendo ya Upendo, na kupanga mipango.
2. **Ombeni pamoja** - Ni kwa nguvu ya Mungu na hekima yake tu tunaweza kubadilisha jamii zetu. Ni kazi isiyowezekana bila Yeye, lakini pamoja naye tunaweza kuleta mabadiliko ya kweli. Kamwe usisahau umuhimu wa maombi; usidanganyike kufikiria kuwa matendo yetu yanatosha bila maombi!
3. **Tathmini mahitaji na uombe** - Kila mtu anapaswa kuja kwenye mkutano tayari kujadili mahitaji yanayowazunguka. Unapokuwa katika mizunguko yako, unapaswa kuangalia mambo yanayohitaji kufanywa au watu wanaohitaji msaada. Kwenye mkutano, jadilini kuhusu nini kifanyike. Ombeni pamoja kwamba Mungu awaoneshe kile mnachopaswa kufanya na awasaidie kupanga mpango utakaomletea Utukufu.
4. **Panga mpango na uombe -** Kwa ujumla, mipango inapaswa kutumia rasilimali ambazo Mungu amekupa na iweze kukamilika kwa muda mfupi**.** Lakini, jambo la muhimu zaidi ni kwamba mipango yako ifuate kile ambacho Mungu amekuonesha ufanye. Biblia inatuambia kwamba njia za Mungu sio njia zetu, hivyo anaweza kukuambia ufanye kitu ambacho hakina maana kwetu kwa sababu kitamletea utukufu atakapokikamilisha.Haikuwa na maana kwa watu katika hadithi kuanza kwa kujenga barabara-kwa kawaida tungeshauri kuanza na mradi mdogo. Lakini, hapo ndipo Mungu alipowaamuru kuanzia, na kadiri walivyofanya, kulikuwa na matokeo makubwa kwenye kijiji chao.
5. **Omba na kisha utekeleze** - Panga tarehe, saa, vifaa, zana, na watu wanaohitajika. Kisha fuata mpango wako.
6. **Tathmini na omba kumshukuru Mungu** - Angalia matokeo na toa sifa kwa Mungu kwa kukusaidia kumaliza kazi hiyo. Katika somo la uwajibikaji, tutajifunza zaidi kuhusu jinsi ya kufanya hatua hii na nini cha kutathmini.

Kumbuka: Shughuli ndogo zinazofanyika mara nyingi ni bora kuliko shughuli moja kubwa ambayo inafanywa mara moja tu. Shughuli ndogo ndogo zinakuruhusu kufanikiwa. Jamii inapokuona unafanya kila wakati vitu

vidogo kuhudumia kuliko shughuli moja tu kubwa kwa mwaka, hii ina tokeo kubwa zaidi kwa jumla. Shughuli moja kubwa itakuwa nzuri, lakini basi, kamwe wasipoona kanisa likiifanyia jamii chochote tena, hivi karibuni litapoteza matokeo yake.

Hitimisho

Katika somo letu linalofuata tutapanga Matendo ya Upendo. Ikiwa unasoma masomo haya kila wiki basi tumia muda wiki hii kumwomba Mungu akuoneshe mahitaji katika jamii ambayo kikundi kinaweza kushughulikia. Uje ukiwa tayari kushirikisha kile ambacho umeona na kile ambacho Mungu amekuwa akikuonesha.

Ikiwa unaenda moja kwa moja kwenye somo linalofuata basi rudia kuangalia notsi zako kwenye somo hili. Ni mawazo gani ambayo umekuwa nayo juu ya kufundisha wengine au Matendo tofauti ya Upendo? Mwombe Mungu akuoneshe mawazo yapi kati ya hayo ambayo anataka ukumbuke unapoendelea na somo linalofuata.

Somo la 8: Mpango wetu wa Matendo

Lengo kuu: Kwa maombi na msaada wa Mungu, tutapanga mpango wa Matendo ya Upendo**.**

Vifaa:

- Mwongozo wa mwanafunzi: hatua za kupanga Matendo ya Upendo

Kupanga Mpango

KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO
Nani anakumbuka hatua za kupanga mpango ambao tuliona katika somo lililopita?

Maelekezo kwa Mwalimu: *Wahimize watu wajaribu na kukumbuka kadiri wanavyoweza. Wakimaliza usome karatasi ya* ***MWONGOZO WA MWANAFUNZI*** *kwa mara nyingine.*

1. **Kutaneni mara kwa mara** - Kama kanisa, mnahitaji mkutane mara kwa mara ili kuzingatia Matendo ya Upendo ili watu wasije wakasahau. Mjaribu kukutana angalau mara moja kwa mwezi kuomba, kujadili Matendo ya Upendo, na kupanga mipango.
2. **Ombeni pamoja** - Ni kwa nguvu ya Mungu na hekima yake tu tunaweza kubadilisha jamii zetu. Ni kazi isiyowezekana bila Yeye, lakini pamoja naye tunaweza kuleta mabadiliko ya kweli. Kamwe usisahau umuhimu wa maombi; usidanganyike kufikiria kuwa matendo yetu yanatosha bila maombi!
3. **Tathmini mahitaji na uombe** - Kila mtu anapaswa kuja kwenye mkutano tayari kujadili mahitaji yanayowazunguka. Unapokuwa katika mizunguko yako, unapaswa kuangalia mambo yanayohitaji kufanywa au watu wanaohitaji msaada. Kwenye mkutano, jadilini kuhusu nini kifanyike. Ombeni pamoja kwamba Mungu awaoneshe kile mnachopaswa kufanya na awasaidie kupanga mpango utakaomletea Utukufu.
4. **Panga mpango na uombe** - Jambo la muhimu zaidi ni kwamba mipango yako ifuate kile ambacho Mungu amekuonesha ufanye. Biblia inatuambia kwamba njia za Mungu sio njia zetu, hivyo anaweza kukuambia ufanye kitu ambacho hakina maana kwetu kwa sababu kitamletea utukufu atakapokikamilisha.
5. **Omba na kisha utekeleze** - Panga tarehe, saa, vifaa, zana, na watu wanaohitajika. Kisha fuata mpango wako.
6. **Tathmini na omba kumshukuru Mungu** - Angalia matokeo na toa sifa kwa Mungu kwa kukusaidia kumaliza kazi hiyo.

Katika somo hili tutafakari kuhusu jambo ambalo Mungu anatutaka tufanye siku zijazo. Ikiwa unakumbuka hadithi ya Kijiji Kilichobadilishwa, utakumbuka kwamba mabadiliko yote yalianza na wao kumwuliza Mungu wafanye nini na, ijapokuwa kazi ilikuwa kubwa - kujenga barabara — waliifanya. Matokeo hayakutarajiwa: waliongeza mapato yao mara kumi, wakaacha kunywa pombe, na wakajikita zaidi katika kutembea kwa utii kwa Mungu katika kila eneo la maisha yao.

Hivyo tuanze leo kwa kuomba na kumwomba Mungu atukumbushe tena mambo ambayo anaweza kuwa anatuambia tuyafanye. Uombea hekima yake unapoangalia orodha ya mawazo mliyoorodhesha pamoja katika 'maeneo 4' sehemu ya somo lililopita na kile Mungu alichokuonesha ulipokuwa ukizunguka wiki hii.

MAOMBI

Maelekezo kwa Mwalimu: *Ongoza kikundi wakati wa sala. Mara tu unapomaliza kumwomba Mungu akupe hekima na akuoneshe mahitaji ambayo anataka uyafikie, tumia muda wa kukaa kimya. Baada ya dakika tano za ukimya, mshukuru Mungu kwamba yuko tayari kutuongoza na kutulinda.*

Waombe watu washirikishe ikiwa wamepata mawazo yoyote wakati walipokuwa kimya. Ikiwa hakuna pitia orodha uliyoandaa katika somo lililopita na kisha angalia kama kuna wazo lolote zuri la kuanzia. Saidia kikundi kuamua kuhusu mradi.

KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO
Sasa kwa kuwa umeamua mradi, sasa tutatumia muda kupanga. Fikiria maswali yafuatayo wakati unapanga mpango.

1. Lini utafanya mradi?
2. Je, kuna rasilimali zozote zinazohitajika? Utazipataje?
3. Je, unahitaji kualika watu washiriki? Nani atafanya hivyo?
4. Unahitaji ruhusa yoyote maalum? Nani ataomba?

Kuendelea kuwa Mwaminifu

KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO
Soma Mathayo 21:28-31

- Katika kifungu hiki kilitokea nini?
- Mtoto yupi alifanya kile ambacho baba alitaka?
    - *Mtoto (Mwana) wa pili. Mwana wa kwanza alimfurahisha baba kwa maneno yake lakini hakuwa na nia ya kuwa mtiifu. Mwana wa pili kweli alifanya kile ambacho baba alimwambia.*
- Hii inamaanisha nini kwetu?
    - *Tunapaswa kukumbuka kuwa haitoshi tu kupanga mipango; tunahitaji kuifuata.*

KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO

- Kuna vikwazo vyovyote vitakavyoweza kukuzuia kutekeleza mpango wako?
- Unaweza kutafanya nini kuvishinda vikwazo hivyo?

MAOMBI
Omba, mkabidhi Mungu mipango yako na uombe msaada wake ili uitimize.

Hitimisho

KIKUNDI KIDOGO CHA MAJADILIANO
Katika vikundi vidogo, angalia ikiwa unaweza kukumbuka wazo kuu moja kutoka kwenye kila somo.

- Mambo gani unayotaka kufanya tofauti kama matokeo ya kusoma moduli hii?

TOA RIPOTI

- Hebu tutumie muda kumshukuru Mungu kwa yote tuliyojifunza katika Moduli hii.
- Nani anataka kuomba na kumwomba Mungu akusaidie kuyatumia yale uliyojifunza?

Somo la9: Kuhamasisha watu Kujitolea

Lengo kuu: Tunahitaji kuhimizana juu ya matendo mema kupitia kufundisha, kutengeneza fursa, kualika watu kushiriki, utambuzi, kufanya kazi kwa pamoja, kuona umuhimu, na kufurahisha.

Vifaa:

- Mwongozo wa Mwanafunzi: Njia Saba za Kuhimiza Kuhudumia
- Mwongozo wa Mwanafunzi: Kanisa linalohudumia
- Jedwali au ubao na chaki/peni.

Maelekezo kwa Mwalimu: *Somo hili limekusudiwa kwa VIONGOZI WA KANISA katika kanisa lako kuwasaidia kufikiria jinsi ya kuwafanya watu wengi katika kanisa lao washiriki katika kuhudumu kanisani au kufanya Matendo ya Upendo.*

Utangulizi: Mtindo wa Maisha ya Kuhudumia

KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO

Katika 1 Wakorintho 12 Paulo anazungumza juu ya mwili wote. Anatukumbusha kwamba sisi WOTE ni viungo vya mwili na, ili mwili ufanye kazi vizuri, viungo vyote vya mwili vinahitaji kutekeleza jukumu lao. Walakini katika makanisa mengine inaonekana kama sehemu tu ya kanisa wanahusika au wanashiriki katika kuhudumu huku wengine wanasubiri kuhudumiwa. Katika somo hili tutaangalia njia mbalimbali za kupata watu wengi wanaoshiriki katika kuhudumia au kuwafanya wale wanaowahudumia wawe na hamasa.

KIKUNDI KIDOGO CHA MAJADILIANO

'Soma Waebrania 10:24: 'Tukaangaliane sisi kwa sisi na kuhimizana katika upendo na matendo mema...'

- Ni njia zipi unazotumia kuimiza watu kushiriki katika kuhudumia? Njia ipi inafanya kazi vizuri? Njia ipi haifanya kazi vizuri?
- Una maoni/mawazo gani mengine ya kuwafanya watu wengi washiriki?
- Unaweza kufanya nini kuwasaidia watu waendelee kuwa na hamasa?

TOA RIPOTI

Kupitia somo hili lote tutaangalia maoni/mapendekezo saba tofauti juu ya jinsi tunavyoweza kuchochea upendo na matendo mema.

Njia saba za kuhamasisha/kuhimiza kuhudumia

Maelekezo kwa Mwalimu: *Unaposoma kila moja, andika ubaoni.*

1. **Fundisha juu ya umuhimu wa kuhudumia**
   Tunahitaji kufundisha kwenye makanisa yetu juu ya umuhimu wa kuhudumia. Ikiwa watu wetu hawajui juu ya wito wa Mungu wa kutumikia jamii zao, hivyo hatuwezi kushangazwa wasipohudumia.
2. **Tengeneza fursa**
   Kwa kuandaa vitu kama Matendo ya Upendo, tunatengeneza fursa kwa watu kanisani kushiriki katika kutumikia. Kwa watu wengine ni vigumu kuona wangeweza kufanya nini, hasa kabla ya kuwa kitu cha kawaida katika maisha ya kanisa. Jaribu kutayarisha fursa mbali mbali ambazo kila mtu mwenye kipaji tofauti aweze kushiriki. Tumia muda kufikiria juu ya vipaji mbalimbali katika kanisa lako na namna ambavyo vinaweza kutumika. Waambie wengine watoe mawazo ya mambo ambayo kanisa linaweza kufanya. Unaweza kushangazwa na ubunifu walio nao.
3. **Waalike watu washiriki**

Watu wengi hawatajitolea kushiriki hadi mtu atanapowaalika. Wanaweza kusikia kutoka kwenye mimbari kile kinachotokea, lakini wanafikiria kuwa watu wengine humo kanisani watafanya. Angalia wale wanaokuzunguka ambao hawashiriki sana kuhudumu na, unapokuwa na Tendo la Upendo au fursa nyingine ya huduma inayolingana na ujuzi wao, basi tumia muda kuwaalika.

4. **Tambua na Washukuru watu**
   Sisi wote tunathamini kutambuliwa na kushukuriwa. Angalia kwa haraka Warumi 16 — ni orodha ndefu ya majina na ya mambo ambayo watu hao walikuwa wamefanya. Je, unaweza kufikiria jinsi walivyojisikia wale waliotajwa katika barua hii kwa kujua kwamba Paulo alikuwa ametambua bidii yao ya kazi na akatumia muda kuorodhesha majina yao kwenye barua hiyo muhimu? Wakati majina haya yanatukumbusha umuhimu wa kufanya kazi kwa bidii, kama viongozi wa kanisa pia tunakumbushwa umuhimu wa kuwatambua na kuwashukuru wengine. Kama viongozi tunapaswa kuhakikisha kuwa tunatumia muda kuwashukuru wale wanaohudumu, hasa wale ambao mara nyingi hawajulikani sana.
5. **Sisitiza umuhimu**
   Soma Mathayo 25: 34-40. Katika njia nyingi hii ni mistari inayostaajabisha. Inatuambia kwamba chochote tunachofanya kwa uchache, ni kana kwamba tunamfanyia Kristo. Matendo yetu ya Upendo ni ya muhimu sana. Tunapoenda kuhudumia, ni kana kwamba tunamfanyia Kristo. Fikiria kwamba ikiwa tungewafikiria wale tunaowahudumia kama Kristo — tungewahudumiaje? Juhudi zetu zingekuwa muhimu kiasi gani? Tunahitaji kuwasaidia watu waone kwamba, wanapotumikia jamii, wanamtumikia Kristo.
6. **Kufanya kazi pamoja**
   Soma hadithi ifuatayo kwa sauti:

Kwa miaka mingi kanisa lilijiuliza ni kwa nini mtu aliyepewa kazi ya kusafisha uwanja wa kanisa angebadilika mara kwa mara. Watu hujitolea na kisha, katika miezi 3 au 4 tu baadaye, wangesema kwamba hawakuweza tena kufanya kazi hiyo. Watu wengi waliojitolea katika maeneo mengine kanisani walikaa kwa miaka mingi katika kazi zao, kwa nini hawa waliojitolea walikuwa wepesi kubadilika? Waliojitolea waliulizwa kwanini waliacha, lakini wengi walisita kutoa jibu kwa uwazi. Wengine walipendekeza kwamba, labda wangekuwa na eneo la timu, ingekuwa bora. Kanisa liliamua inafaa kujaribu, hivyo timu ya bustani iliundwa.

Leo kuna idadi ya wakina baba, watoto wa kiume na wanaume wengine kwenye timu ya bustani. Wanakutana pamoja kila Jumamosi saa 7 asubuhi. Wanaanza na sala, kisha wanaelekea sehemu mbali mbali za kufanyia kazi wakiwa wawili wawili — watu 2 kukatia miti, 2 kufagia. Saa 3 asubuhi wanakunywa kahawa pamoja na kushirikishana juu ya mambo yanavyoenda katika maisha yao. Kila mtu ana nafasi ya kushirikisha, na wanamaliza kwa maombi. Kisha hurudi kuendelea kufanya kazi pamoja. Sasa watu wanakaa kama sehemu ya timu ya bustani kwa miaka mingi. Wanaondoka wakati wanapokuwa na shida ya kiafya au wana majukumu mengine.

Jadili:

- Ni jambo gani liliwafanya waliojitolea wafanye kazi kwa moyo mmoja kwa muda mrefu zaidi?
- Kwa nini unafikiria kwamba kutumikia/kuhudumia kwa pamoja ni muhimu sana?
- Ni mambo gani ambayo walifanya ili kujenga umoja?
- Kuna mawazo gani ya jinsi tunavyoweza kusaidia watu kuhudumu pamoja?

7. **Kuwe kunafurahisha**
   Watu watafanya mambo zaidi wanayoona yanafurahisha! Watafanya kazi kwa muda mrefu na watajihusisha zaidi wanapofurahia kile wanachofanya. Wakati mwingine tunafikiria kuwa mambo ya Kikristo yanapaswa kufanywa kwa uzito bila utani, lakini mara nyingi Biblia inazungumzia juu ya furaha. Mbinguni patakuwa mahali palipojazwa furaha.

KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO

Maelekezo kwa Mwalimu: *Tumia* ***MWONGOZO WA MWANAFUNZI.***

- Je, umejaribu njia yoyote kati ya hizi? Njia ipi imefanya kazi? Njia ipi haikufanya kazi?

- Ni vifungu gani ambavyo tunaweza kutumia kufundishia umuhimu wa huduma?
- Ni njia zipi ambazo umetumia kuwatambua na kuwashukuru watu? Mawazo gani mengine ambayo unaweza kujaribu?
- Unawezaje kutengeneza furaha/raha zaidi? Ni njia gani za kufanya kutumikia au kuhudumia kufurahishe zaidi?

TOA RIPOTI
Maelekezo kwa Mwalimu:*Hakikisha unawapa muda wa kutosha wa kujibu maswali haya na kutoa ripoti.*

SHUGHULI YA KIKUNDI KIKUBWA
Tumeona njia saba ambazo zinawatia moyo au kuwahamasisha watu kushiriki katika kuhudumia: kufundisha, kutengeneza fursa, kuwaalika watu washiriki, kutambuliwa, kufanya kazi pamoja, kuona umuhimu, na kufurahisha.

Maelekezo kwa Mwalimu: *Mwambie kila mtu aje mbele na kuweka alama karibu na vitu 3 ambavyo vingewahamasisha zaidi.*

- Je, kila mtu alichagua njia sawa? *Kwa kawaida watakuwa tofauti.*
- Eleza kwamba watu wote wanahamasika tofauti, kwa hiyo katika makanisa yetu tunahitaji kuweka mpango kwa pamoja ambao unahamasisha kila aina za watu.
- Je, kuna wowote waliopata alama za juu sana? Kwa nini unafikiri hawa walipata alama nyingi zaidi? Je, kuna njia ambazo unatumia njia hii kuwatia moyo watu katika kanisa lako?

Kanisa linalohudumia

Tukitaka makanisa yetu kukuza mtindo wa maisha wa kufanya Matendo ya Upendo mara kwa mara (sio mara moja tu kwa wakati), basi kwanza tunahitaji kuombea kanisa letu. Kisha tunahitaji kufanya kile tunachoweza kuzungumza, kufanya, na kusherehekea Matendo ya Upendo mara kwa mara. Sikiliza hadithi hii ya kanisa lililofanya bidii kufanya Matendo ya Upendo kuwa sehemu ya maisha kwa kanisa lao.

Mchungaji James alikuwa akihisi ameshindwa kidogo. Alijua kwamba alitaka apate watu wanaohudumu katika kanisa lake, lakini hakujua ni kwa namna gani. Rafiki alikuwa amempa namba ya simu ya Mchungaji Moses na akapendekeza kwamba ampigie kwa ushauri. Alimpigia Mchungaji Moses na baada ya mazungumzo mafupi aliambiwa kwamba anahitaji kujenga mazingira ya kuhudumia kanisani kwake. Mchungaji James ilibidi akiri kwamba hakujua mazingira ya kuhudumia yalikuwaje. *'Usijali,'* Mchungaji Moses alijibu*, "hata mimi sikujua hadi miaka michache iliyopita. Njoo kwenye moja ya huduma zetu, nami nitakuonesha ninachomaanisha. '*

Mchungaji James alikutana na Mchungaji Moses kwenye mlango wa kanisa. Alifarijika na akafurahi kuona kwamba Mchungaji Moses alionekana kweli anataka kumsaidia kuliko kumwonesha tu kanisa lake kubwa.

Walipoingia kanisani, Mchungaji James aliona bango kubwa. Iiliandikwa "Shirikishi katika Siku ya Kuhudumia." Chini ya kichwa cha tangazo kulikuwa na aya '… lakini ninyi, ndugu, msikate tamaa katika kutenda mema. - 2 Wathesalonike 3:13. 'Chini ya hii, kila mwezi iliorodheshwa mistari 3 chini yake. Mstari wa kwanza ulikuwa wa idadi ya Matendo ya Upendo yaliyokuwa yamefanywa mwezi huo, mstari wa pili, idadi ya watu waliosaidiwa, na mstari wa tatu, idadi ya watu waliokuwa wameshiriki katika kusaidia.

'Hii ni nini?' Mchungaji James aliuza.

'Tuna siku ya kuhudumia kila mwezi,' Mchungaji Moses alielezea. 'Siku hizo tunajaribu kupata watu wengi kanisani wa kuhudumu kadiri iwezekanavyo. Mara kwa mara mimi hualika watu wajiandikishe ninapohubiri, na watu katika kanisa wanawaalika wengine wanaokutana nao kwenye maisha ya kila siku. Wengine huhudumu kanisani kwa kusaidia kwenye bustani au kupaka rangi chumba. Wengine wanahudumia jamii kwa kukarabati nyumba au kuwafurahisha watoto. Tunayo matangazo kadhaa kulizunguka kanisa ya kuwakumbusha watu juu ya siku hizi na kuwasaidia kuona ni watu wangapi wanahudumia na kwamba bado

tunawahitaji washiriki. Kila mwezi tunaandika idadi ya Matendo ya Upendo tuliyoweza kufanya, idadi ya watu waliosaidiwa, na idadi ya watu waliohusika/walioshiriki. Kila mwezi, tunajaribu kuongeza idadi ya watu wanaoshiriki. '

Mchungaji James alipotazama kuzunguka kanisa, aligundua kuwa ilikuwa kweli — kulikuwa na mabango kadhaa yenye aya mbalimbali kwenye kuta. Kwenye ukuta wa nyuma kulikuwa na picha kadhaa za matukio ya kuhudumia yaliyotokea zamani. Kulikuwa na picha nyingi za watu walioshiriki katika mambo mbalimbali: kujenga nyumba, kurekebisha barabara, kusafisha kanisa, na kufundisha watoto. Juu ya picha hizo kulikuwa na maneno makubwa yaliyosomeka, 'Tujenge Ufalme wa Mungu pamoja.'

Mchungaji James alikaa kitini wakati Mchungaji Moses akijiandaa kuanza ibada. Mchungaji James aliona watu wenye ukarimu wakisalimia kila mtu mlangoni na mwanamke akiwasaidia vipofu na wazee kupata viti na kuwahudumia chai. Alihisi kukaribishwa sana katika kanisa hili na alijiuliza kama angeweza kufanya kitu kama hicho katika kanisa lake.

Ibada ilipoanza, vijana kucheza na waumini waliimba nyimbo. Baada ya muda wa kuabudu, Mchungaji Moses aliwaalika watu kutoa ushuhuda. Mwanamke mzee alikuja mbele na kutoa ushuhuda, 'Nimefiwa na mume wangu na sasa ninamtunza mjukuu wangu wa kiume mwenyewe. Nyumba yangu ilikuwa katika matengenezo duni na ilivuja vibaya na mjukuu wangu alikuwa akifanya vibaya shuleni. 'Ghafla, alitabasamu sana,' Sasa kanisa limekuja na kunisaidia kukarabati paa. Na baadhi ya vijana walimwalika mjukuu wangu awe sehemu ya programu ya kufundisha ili asifanye vibaya shuleni. Ninashukuru sana kwa namna ambavyo kanisa limenijali. Asanteni wote! 'Kila mtu aliguswa na ushuhuda huo. Mchungaji Moses alirudi mbele ya kanisa na kuziomba timu zilizokarabati nyumba na kufundisha kusimama. Walipofanya hivyo kanisa lote liliwashangilia kwa nguvu. Walionekana kufurahi na kukaa kwa haraka.. Mchungaji Moses aliomba sala ya haraka kwa mwanamke huyo na timu zilizohudumia- kumshukuru Mungu kwa utayari wao wa kusaidia, kumshukuru Mungu kwa kuwatumia, na kumwomba Mungu aendelee kulisaidia kanisa kumletea utukufu kwa matendo yao ya huduma. Kisha Mchungaji Moses alikumbusha kanisa kwamba siku nyingine ya kuhudumia ilikuwa wiki 2 zijazo. Aliwaambia kwamba wanahitaji mwili wote/kanisa lote lifanye kazi pamoja ili kujenga Ufalme wa Mungu. Aliwakumbusha kwamba hakukuwa na sehemu za mwili zisizo na kazi na kwamba, kama mwili wa mwanadamu, kukiwa na sehemu zisizofanya kazi, basi mwili wote haufanyi kazi vizuri kama unavyoweza. Kisha akawaomba wale waliokuwa wameshajiandikisha kuhakikisha kwamba wote wanamwomba mtu ajiunge nao siku ya kuhudumia.

Ibada ilipoendelea, Mchungaji James alizingatia yote aliyokuwa ameyaona na kuyasikia. Je, kulikuwa na mshangao wowote kwamba watu wengi kutoka kanisa hili walishiriki katika Matendo ya Upendo mara kwa mara? Mwishowe alielewa kile ambacho Mchungaji Moses alimaanisha aliposema kwamba lazima ujenge mazingira ya kuhudumia.

Maelekezo kwa Mwalimu: *Tumia* ***MWONGOZO WA MWANAFUNZI.***

- Njia saba za kuhimiza au kuhamasisha zimewasilishwaje katika hadithi hii?
- Ni mawazo gani mengine unaweza kujifunza yanayoweza kufanya kazi vizuri katika kanisa lako?

Hitimisho

Waefeso 4 inasema: 'Mwili wote… hukua na kujijenga katika upendo kama kila sehemu inavyofanya kazi yake.' Tunakua kadiri tunavyopewa fursa ya kutumia vipaji vyetu! Kama viongozi tunataka kuhimiza kanisa lote kushiriki katika kuhudumu.

TAFAKARI BINAFSI

Angalia tena njia saba za kuhamasisha wengine kuhudumia na mawazo ambayo yametolewa katika vikundi. Ni mambo gani matatu unayotaka kuyatekeleza mwezi huu ili kupata watu wengi katika kanisa lako washiriki katika kuhudumia?

Maelekezo kwa Mwalimu: *Maliza kwa kutumia muda kuombea makanisa yao na kuombeana wao kwa wao.*